

**MAKOSA YA KIFONOLOJIA YANAYOFANYWA NA WAZUNGUMZAJI  
WA KIHAYA WANAOFUNZA KISWAHILI SANIFU: MFANO KUTOKA  
BUKOBANISPAA**

**FREDERICK FELICIAN**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA  
KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO  
KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

## UTHIBITISHO

Aliyeweka saina hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa: ***Makosa ya Kifonolojia Yanayofanywa na Wazungumzaji wa Kihaya Wanaojifunza Kiswahili Sanifu:*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya Kukamilisha masharti ya shahada ya MA. Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

---

Dkt. Salma O. Hamad

**(Msimamizi)**

---

Tarehe

## **HAKIMILIKI**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri kwa mfumo wowote ule au kutoa hata sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii na / au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**TAMKO**

Mimi **Frederick Felician**, ninatamka na kuthibitisha kwamba Tasnifu hii iitwayo: *Makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu* ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa popote pale kwa lengo la kutunukiwa shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

---

Sahihi

---

Tarehe

**TABARUKU**

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa mama yangu mzazi Magreth Felician kwa kuniwezesha kupata elimu tangu elimu ya msingi mpaka sasa, mke wangu wapendwa Johnmary na wanangu Bryan Mutegeki na Karen Ainekisha mna kila sababu ya kuhakikisha kuwa mnapata elimu ili iwe ufunguo wa maisha yenu.

## SHUKURANI

Mtu bila Mungu na watu si mtu. Singeikamilisha safari ya kuandaa kazi hii bila uwepo wa mikono yako. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kunipa nguvu za kukabiliana na vizingiti mbalimbali wakati wa kutafitia mada hii. Nguvu na afya njema uliyonijalia imesukuma mbele kazi hii.

Shukurani za pekee ninampa msimamizi wangu mpendwa Dkt. Salma Hamad kwa kuutumia muda wake, kwa hali na mali katika kunitia moyo nilipoonekana kukata tamaa. Licha ya mapungufu niliyokuwa nayo aliweza kunivumilia, akaipitia kazi yangu, akaisahihisha na kunielekeza vilivyo ili kuhakikisha kuwa inakuwa inavyotakiwa kuwa. Ulinivumilia na kunihimiza nitie bidii ili kuikamilisha kazi hii kwa muda. Umenifunza mengi sio tu katika utafiti huu bali pia katika maisha kwa ujumla. Mungu ambariki sana huyu mama!

Ninakishukuru Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii wakiwemo walimu wangu Dkt. Zelda Elisifa, Dkt Mohamed Omary, Dkt. Hanna Simpassa, Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Nestory Ligembe na Dkt. Dunlop Ochieng kwa taaluma, maarifa na ushauri walionipa na kwa ushirikiano mzuri ulioniwezesha kukamilisha kazi hii. Nasema asante sana, Mungu awajaalie afya njema ili mwendelee kutenda mema.

Ninapenda kumshukuru sana mke wangu mpendwa Johnmary Rutakumwa Joseph kwa ushauri wako kwangu na mchango wako wa kifedha katika masomo yangu. Umenitia moyo hasa pale nilipokata tamaa, Mungu ambariki sana na kumshindia katika yote. Aidha, ninawashukuru sana watoto wangu wapendwa Bryan Mutegeki na

Karen Ainekisha kwa kunivumilia kwani kipindi ambacho sikuwepo walikuwa wakikosa upendo wa baba.

Ninamshukuru mama yangu mzazi Magreth Felician kwa kunishauri, kuniombea mafanikio na kunitia moyo katika safari ya masomo yangu haya. Kaka yangu Evodius Musinga na wadogo zangu Dickson Felician na Eliud Felician kwa ushauri wao na misaada yao ya hali na mali waliyonipa ili kuhakikisha kuwa ninafaulu. Wabarikiwe mno!

Ninajua kuna wengi waliochangia ambao sijawataja kwa ukosefu wa nafasi. Kwao wote ninasema asanteni sana na Mungu awabariki!

## IKISIRI

Utafiti huu umechunguza wa makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Malengo ya Utafiti huu yalikuwa ni (a) Kubainisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu (b) Kubainisha sababu za wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa ya kifonolojia katika kujifunza Kiswahili sanifu (c) Kubainisha mbinu za kutumia ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu kama L2 kwao. Njia zilizotumika kukusanya data ni hojaji ilitumika kwa watafitiwa ambao ni wanafunzi, walimu na wazazi, mahojiano ambayo ilitumika kwa walimu na wazazi wazungumzaji wa Kihaya na Kiswahili na usomaji makini ambayo ilitumika kupitia kwa umakini kazi mbalimbali za wanafunzi ili kubaini makosa ya kifonolojia. Data ya utafiti huu imechanganuliwa kwa makabala wa kimaelezo kwa kuongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder (1967). Matokeo ya utafiti yanaonesha makosa yanayofanywa kuwa ni pamoja na matumizi ya sauti mbadala kwa sauti ambazo hazipo katika mfumo wa lugha ya Kihaya ila zipo katika Kiswahili sanifu, kuchanganya sauti, udondoshaji na uchopekaji wa sauti. Sababu za wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa ya kifonolojia katika kujifunza Kiswahili sanifu zipo kama ifuatavyo; utofauti wa mifumo ya sauti kati ya lugha hizi mbili, ufundishaji mbaya wa lugha ya pili, walimu kutokuwa na taaluma ya fonetiki matamshi na matumizi ya Kihaya muda mwingi kwa walimu, wanafunzi na jamii kwa ujumla. Mbinu za kuwasaidia wanafunzi hawa ni pamoja na wazazi, wanafunzi na jamii nzima ya wazungumzaji wa lugha ya Kihaya kutambua umuhimu wa Kiswahili, taaluma ya fonetiki matamshi kutolewa ngazi zote za elimu, matumizi ya mbinu bora za ufundishaji wa lugha ya pili.



## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHO</b> .....	<b>ii</b>
<b>HAKIMILIKI</b> .....	<b>iii</b>
<b>TAMKO</b> .....	<b>iv</b>
<b>TABARUKU</b> .....	<b>v</b>
<b>SHUKURANI</b> .....	<b>vi</b>
<b>IKISIRI</b> .....	<b>viii</b>
<b>ORODHA YA VIELELEZO</b> .....	<b>xiv</b>
<b>ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA</b> .....	<b>xv</b>
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	<b>1</b>
<b>UTANGULIZI WA JUMLA</b> .....	<b>1</b>
1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Usuli wa Mada .....	1
1.2.1 Kiswahili.....	2
1.2.2 Kihaya.....	3
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .....	4
1.4 Malengo ya Utafiti .....	5
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti .....	5
1.4.2 Malengo Mahsusi .....	5
1.5 Maswali ya Utafiti.....	5
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.7 Upeo wa Utafiti.....	7
1.8 Muhtasari .....	8

<b>SURA YA PILI .....</b>	<b>9</b>
<b>MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA .....</b>	<b>9</b>
2.1 Utangulizi .....	9
2.2 Maana ya Fonolojia, Fonolojia ya Kiswahili na Fonolojia ya Kihaya.....	9
2.2.1 Maana ya Fonolojia.....	9
2.2.2 Fonolojia ya Kiswahili .....	10
2.2.3 Sauti Konsonanti za Kiswahili Sanifu .....	10
2.2.2.1 Sauti Irabu za Kiswahili Sanifu .....	18
2.2.3 Fonolojia ya Kihaya .....	20
2.2.3.1 Sauti Konsonanti za Lugha ya Kihaya .....	20
2.2.3.2 Sauti Irabu za Lugha ya Kihaya.....	26
2.2.4 Silabi .....	28
2.2.4.1 Miundo ya Silabi za Kiswahili Sanifu .....	28
2.2.4.2 Muundo wa Silabi za Lugha ya Kihaya .....	31
2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Ujifunzaji wa Lugha na Uhusiano Wake wa Kuathiriana .....	33
2.4 Nadharia ya Utafiti.....	37
2.5 Muhtasari.....	40
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>42</b>
<b>MBINU NA NJIA ZA UTAFITI.....</b>	<b>42</b>
3.1 Utangulizi .....	42
3.2 Aina ya Utafiti .....	42
3.3 Eneo la Utafiti.....	42
3.4 Sampuli na Usampulishaji.....	43

3.4.1	Sampuli.....	43
3.4.2	Mbinu za Usampulishaji.....	44
3.5	Njia za Ukusanyaji wa Data .....	46
3.5.1	Hojaji au Dodoso .....	46
3.5.2	Mahojiano.....	48
3.5.3	Usomaji Makini .....	49
3.6	Vifaa vya Kukusanyia Data.....	49
3.7	Uchambuzi wa Data .....	50
3.8	Muhtasari.....	51
	<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>52</b>
	<b>UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA .....</b>	<b>52</b>
4.1	Utangulizi .....	52
4.2	Utambuzi wa Makosa.....	53
4.3	Uchambuzi wa Makosa .....	58
4.3.1	Matumizi ya Sauti Mbadala.....	58
4.3.1.1	Matumizi ya Sauti /g/ Badala ya /gh/.....	58
4.3.1.2	Matumizi ya Sauti /s/ Badala /th/.....	59
4.3.1.3	Matumizi ya Sauti /z/ Badala ya /dh/ .....	60
4.3.1.4	Matumizi ya Sauti /ng/ Badala ya /ngø/.....	60
4.3.2	Kuchanganya Sauti .....	61
4.3.2.1	Kuchanganya Sauti /a/ na /h/ .....	61
4.3.2.2	Kuchanganya Sauti /r/ na Sauti /l/ .....	62
4.3.2.3	Kuchanganya Sauti /th/ na Sauti /dh/.....	63
4.3.2.4	Kuchanganya Sauti /a/ na /w/ .....	63

4.3.3	Uchopekaji wa Sauti .....	64
4.3.3.1	Uchopekaji wa Sauti /h/ .....	64
4.3.3.2	Uchopekaji wa Sauti /u/ na /i/ Katika Silabi Funge Silabi za Konsonati Pekee .....	65
4.3.4	Udondoshaji wa Sauti .....	66
4.3.4.1	Udondoshaji wa Sauti /h/ .....	67
4.3.4.2	Udondoshaji wa sauti /u/ .....	68
4.4	Sababu za Kufanya Makosa ya Kifonolojia .....	68
4.5	Mbinu za Kutumia ili Kuwasaidi Wazungumzaji wa Kihaya Wanaojifunza Kiswahili Sanifu .....	74
4.6	Muhtasari.....	77
	<b>SURA YA TANO.....</b>	<b>78</b>
	<b>MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO .....</b>	<b>78</b>
5.1	Utangulizi .....	78
5.2	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .....	78
5.3	Mapendekezo ya Utafiti .....	79
5.4	Hitimisho .....	80
	<b>MAREJELEO.....</b>	<b>81</b>
	<b>VIAMBATANISHO .....</b>	<b>85</b>

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 2.1: Uainishaji wa Konsonanti kwa Kutumia Vigezo vya Uainishaji wa Konsonanti za Kiswahili Sanifu.....	16
Jedwali Na. 2.2: Sauti Konsonanti za Kiswahili sanifu.....	17
Jedwali Na. 2.3: Sauti Irabu za Kiswahili Sanifu.....	19
Jedwali Na. 2.4: Uainishaji wa Konsonanti kwa Kutumia Vigezo vya Uainishaji wa Konsonanti za Lugha ya Kihaya .....	25
Jedwali Na. 2.5: Sauti Konsonanti za Kihaya .....	25
Jedwali Na. 2.6: Sauti Irabu za Kihaya.....	27
Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Watafitiwa .....	45
Jedwali Na. 4.1: Kuonesha Matumizi ya Sauti /g/ .....	58
Jedwali Na. 4.2: Kuonesha Matumizi ya Sauti /s/.....	59
Jedwali Na. 4.3: Kuonesha Matumizi ya Sauti /z/ .....	60
Jedwali Na. 4.4: Kuonesha Matumizi ya Sauti /ng/ .....	60
Jedwali Na. 4.5: Kuonesha Matumizi ya Sauti /a/ .....	61
Jedwali Na. 4.6: Kuonesha Matumizi Ya Sauti /r/ .....	62
Jedwali Na. 4.7: Kuonesha Matumizi ya Sauti /th/ .....	63
Jedwali Na. 4.8: Kuonesha Matumizi ya Sauti /a/ .....	64
Jedwali Na. 4.9: Kuonesha Matumizi ya Sauti /h/ .....	65
Jedwali Na. 4.10: Kuonesha Uchopekaji wa Sauti /u/ na /i/ .....	66
Jedwali Na. 4.11: Kuonesha Matumizi ya Sauti /h/ .....	67
Jedwali Na. 4.12: Kuonesha Udondoshaji wa Sauti /u/.....	68

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 2.1: Kielelezo cha Kuonyesha Ulimi Wakati wa Utamkaji wa Irabu....	19
Kielelezo Na. 4.1: Kuonesha Matumizi ya Sauti /g/ Badala ya Sauti /gh/ .....	54
Kielelezo Na. 4.2: Kuonesha Matumizi ya Sauti /ng/ Badala ya Sauti /ngø/ na Uchopekaji wa Sauti /u/ .....	54
Kielelezo Na. 4.3: Kuonesha Matumizi ya Sauti /z/ Badala ya Sauti /dh/ .....	55
Kielelezo Na. 4.4: Kuonesha Matumizi ya Sauti /s/ Badala ya Sauti /th/.....	55
Kielelezo Na. 4.5: Kuonesha Udondoshaji wa Sauti /h/.....	56
Kielelezo Na. 4.6: Kuonesha Udondoshaji wa Sauti /u/.....	56
Kielelezo Na. 4.7: Kuonesha Uchopekaji wa Sauti /h/ na /u/ .....	57
Kielelezo Na. 4.8: Kuonesha Kuchanganya Sauti /l/ na /r/.....	57

**ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA**

#	Mipaka ya neno
\$	Mipaka ya silabi
//	Mabano ya fonetiki
K.K.K.	Kusoma, Kuandika na Kuhesabu
L1	Lugha ya kwanza
L2	Lugha ya pili

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI WA JUMLA**

#### **1.1 Utangulizi**

Utafiti huu umechunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Tasnifu ya utafiti huu ina sura kuu tano. Sura ya kwanza ni usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti. Sura ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi na nadharia ya utafiti. Sura ya tatu inaelezea mbinu za utafiti. Sura ya nne ni uwasilishaji na uchambuzi wa data na sura ya tano ni muhtasari, mapendekezo na hitimisho.

#### **1.2 Usuli wa Mada**

Utafiti huu umechunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Hawa ni wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili huku lugha yao ya kwanza ikiwa ni lugha ya Kihaya. Wanaisimu wengi wamefanya tafiti zao kuhusiana na namna binadamu anavyojifunza lugha kwa kujikita katika lugha za kigeni. Tafiti hizo zinaonyesha mchango wa makosa katika kujifunza lugha ya pili na hata chanzo cha makosa hayo (Corder 1971, Jain 1974, Richard 1971, Richard na Sampson 1974).

Makosa katika lugha ni hali ya mtu kushindwa kutamka neno au fungu la maneno kwa ufasaha kutokana na kukosa umahiri katika lugha lengwa. Makosa katika lugha huchunguzwa kwa mtu anayezungumza lugha zaidi ya moja ambapo sifa za lugha moja huingilia sifa za lugha nyingine kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia (Richard 1971). Aidha makosa katika lugha hutokana na mtu kutozingatia kanuni na taratibu za



lugha lengwa wakati wa mazungumzo au kuandika. Hii husababisha kutamka au kuandika neno lisilokuwepo katika lugha lengwa na wakati mwingi kutoa ujumbe usiokusudiwa kutoka kwa mzungumzaji au mwandishi.

Mara nyingi makosa katika lugha hufanywa na mtu anayejifunza lugha bila ya yeye kujua kama anatenda makosa katika lugha lengwa. Kwa mfano wanafunzi walio wengi hutamka sauti za lugha ya pili kwa kuzingatia vitamkwa vya lugha yao ya kwanza (Richard and Sampson 1974). Hivyo makosa katika lugha utambulika kama kosa iwapo mzungumzaji au mwandishi wa lugha lengwa atarudia kosa hilo zaidi ya mara moja.

Utafiti huu umechunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Utafiti huu umebainisha na kuainisha makosa, kueleza sababu ya kosa na kueleza mbinu mbadala zinazoweza kutumika kuwasaidia wazungumzaji wa kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Kwa machache ni vizuri kusema kuhusu lugha ya Kiswahili na lugha ya Kihaya.

### **1.2.1 Kiswahili**

Ali (2013) anasema Kiswahili ni lugha moja miongoni mwa lugha za Kibantu inayozungumzwa katika bara la Afrika, hasa Afrika Mashariki yenye asili ya watu wa mwambao. Massamba (2002:35-36) anasema kuwa mwanazuoni wa kwanza kutafiti lugha za Kibantu ni Wilhelm. H. I Bleek, ambaye katika uainishaji wake aliweka lugha ya Kiswahili katika kundi la Zangi, kundi la Kaskazini Mashariki ambalo kwa mujibu wa utaratibu alioufuata lilikuwa ni kundi mojawapo kati ya makundi ya tawi la kati la lugha za Kibantu. Bleek alionyesha dhahiri kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwa na

sifa zote kuu zilizopatikana katika lugha nyingine za Kibantu kwa ujumla. Massamba (ameshatajwa) anaendelea kusema kuwa mwanazuoni mwingine aliyedhihirisha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu ni Malcom Guthrie katika miaka ya (1967, 1970, 1971). Katika uainishaji wake lugha ya Kiswahili iliangukia katika Kanda G10 na ilipewa kitambulisho cha G42.

Nchimbi (2008:169) anasema Kiswahili ni lugha ya wenyeji wa pwani ya Afrika mashariki lakini kutokana na mwingiliano wa wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki na wenyeji wa bara Kiswahili kiliweza kuenea kutoka pwani ya Afrika Mashariki kuingia bara ya Afrika Mashariki. Waarabu na Wakoloni walipoingia Afrika Mashariki walikuta Kiswahili kimeishaenea maeneo mengi ya Afrika Mashariki. Hivyo, wakaamua kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao. Waarabu na Wakoloni walisaidia Kiswahili kuenea nje ya mipaka ya Afrika Mashariki mpaka Rwanda, Burundi, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Baada ya Uhuru Kiswahili kilitewiwa kuwa lugha rasmi na lugha ya taifa Nchini Tanzania. Massamba na wenzake (2001) wanasema lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya taifa katika nchi za Tanzania na Kenya. Katika Tanzania ndiyo lugha inayotumiwa takribani katika shughuli zote rasmi mijini na vijijini.

### **1.2.2 Kihaya**

Kwa upande wa Kihaya, Theophil (2012) anasema Ki (Ru) haya ni lugha mojawapo ya lugha za Kibantu inayozungumzwa Kaskazini Magharibi mwa Tanzania, ukanda wa Magharibi wa mwambao wa ziwa Victoria. Lugha hii inazungumzwa na wakazi wa wilaya ya Bukoba mjini, Bukoba vijijini, Muleba na sehemu chache za wilaya ya Karagwe ambazo ni kata ya Kaisho, vijiji vya Karukwanzi, ishaka, Isingiro, Katera na

Nyabishenge. Kwa upande wa Kata ya Nkwenda, lugha ya Kihaya inazungumzwa katika vijiji vya Nkwenda, Rwabwera, Itera na Chanya.

Jamii ya Wahaya kwa mujibu wa Mradi wa Lugha za Tanzania (2009), inaishi katika ukanda wa ziwa Victoria, mkoa wa Kagera. Jamii hii hujitambulisha kwa lugha yake ya asili ya Kihaya ambayo ni miongoni mwa lugha zisizopungua mia moja na hamsini (150) zinazounda jamii ya Watanzania.

Lugha ya Kihaya ni lugha ya kwanza kwa Wahaya ambao hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili kwao na kuitumia kama lugha ya Taifa na lugha rasmi. Kwa kuzingatia hayo yaliyosemwa kuhusu lugha ya Kiswahili ni dhahiri kwamba lugha hii ni lugha muhimu sana na ina mawanda mapana kimatumizi tofauti na lugha ya Kihaya.

### **1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti**

Utafiti huu umechunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Hii ni kutokana na kazi mbalimbali alizosoma mtafiti hakukutana na utafiti wowote uliwahi kufanyika kama huu. Mtafiti alishawishika kufanya utafiti huu baada ya kugundua Wahaya hawatamki Kiswahili sanifu inavyotakiwa. Mtafiti aliona kuwa inawezekana kuna tatizo kwenye kipengele cha kifonolojia kati ya lugha hizi mbili.

Kwa hiyo utafiti huu umeweza kubainisha makosa ya Kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili kwao, sababu za kufanyika kwa makosa hayo na mbinu za kuwasaidia.

## **1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na malengo ya aina mbili, nayo ni lengo kuu na malengo mahsusi.

### **1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti**

Kuchunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

### **1.4.2 Malengo Mahsusi**

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi matatu.

- (i) Kubainisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu.
- (ii) Kubainisha sababu za wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa ya kifonolojia katika kujifunza Kiswahili sanifu.
- (iii) Kubainisha mbinu za kutumia ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili.

## **1.5 Maswali ya Utafiti**

- (i) Ni makosa gani ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu?
- (ii) Je, nini kinasababisha wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa hayo katika kujifunza Kiswahili sanifu?
- (iii) Mbinu gani zitumike ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Utafiti huu una umuhimu mkubwa kwa wanaisimu kama ifuatavyo:

Moja, Umesaidia kutambua athari za kimatamshi za lugha ya Kihaya na jinsi zinavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya utafiti huu imeweza kubainisha makosa ya kifonolojia ya lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili na kuweka wazi makosa hayo.

Pili, Matokeo ya utafiti huu yatawasidia walimu kufahamu sehemu za lugha ambazo huwatatiza wanafunzi hivyo kuzitilia mkazo zaidi. Pia, watanufaika na mikakati ya kukabili makosa haya ambayo imependekezwa na utafiti huu.

Tatu, kuna mitazamo hasi miongoni mwa wanajamii kuwa mwanafunzi anapofanya makosa katika mazungumzo au katika uandishi wake hiyo ni ishara ya udhaifu na kushindwa maishani. Matokeo ya utafiti huu yatachangia katika kurekebisha mitazamo ya jinsi hiyo kwa kuyafungamanisha na maoni ya wataalam mbalimbali kama vile Corder (1967). Mtaalam huyu anashauri kwamba makosa yanayojitokeza mtu anapojifunza L1 na L2 ni jambo la kawaida kutokea kabla ya mtumiaji wa lugha kuzoea matumizi kamili ya kanuni za lugha lengwa. Kulingana naye, kufanya makosa ni jambo la kawaida.

Kwa hivyo, mwanafunzi anapofanya makosa asiadhibiwe bali makosa hayo yachukuliwe kama kigezo cha kuthibitisha kwamba bado mwanafunzi husika hajafikia umilisi wa lugha lengwa. Utafiti huu vilevile, umewapa changamoto walimu wenye msimamo wa namna hii kuzua mbinu mbadala za kuwasaidia wanafunzi.

Nne, utafiti huu utatumika kama marejeleo kwa watafiti wengine watakaochunguza athari za lugha za kibantu katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu. Vile vile utakuwa marejeleo kwa watafiti mbalimbali watakaochunguza kuathiriana kwa L1 na L2.

### **1.7 Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu ulijihusisha na uchambuzi wa makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu. Kijiografia utafiti huu ulifanyika katika mkoa wa Kagera wilaya ya Bukoba Manispaa katika kata ya Ijuganyondo, kata ya Kahororo, kata ya Buhembe na kata ya Kitendaguro. Sababu ya kuchagua kata za pembezoni ya mji ni kwa sababu kata za mjini katikati wanafunzi walio wengi hutumia lugha ya Kiswahili mara kwa mara wawapo shuleni na hata nyumbani. Baadhi yao hutumia Kiswahili kama lugha ya kwanza. Hivyo, iwapo ningelichagua kata za mjini katikati nisingeliweza kupata data iliyo sahihi na ya uhakika. Shule zilizohusika katika utafiti huu ni shule ya msingi Ibura iliyopo kata Ijuganyondo, Kitendaguro na Bugambakamoi zilizopo kata Kitendaguro, Kahororo iliyopo kata Kahororo, na shule ya Msingi Kashenge iliyopo kata Buhembe.

Mipaka kitaaluma, makosa yaliyochunguzwa ni makosa ya kifonolojia hususani matamshi ya lugha ya Kihaya yanavyoathiri wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili. Wanafunzi waliotafitiwa ni wanafunzi wa darasa la nne na darasa la tatu tu. Nimechagua wanafunzi wa darasa la tatu na la nne kwa sababu wanafunzi wa madarasa hayo tayari wameishajifunza masuala ya Irabu, konsonanti, na silabi wakati wakiwa darasa la kwanza na la pili. Pia ndiyo wanafunzi waliopitia katika muhtasari

wa darasa la kwanza na la pili unaosisitiza kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) katika Kiswahili sanifu.

### **1.8 Muhtasari**

Katika sura hii ya kwanza, mtafiti ameweka bayanausuli wa mada juu ya ujifunzaji wa pili na makosa yanayotokana nayo. Pia amejadili kuhusu ya Kiswahili na Kihaya. Vilevile amejadili tamko la utafiti wake kwa kuonesha pengo la utafiti. Malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti yamewekwa bayana. Mtafiti ameeleza kwa kina umuhimu wa utafiti wake pamoja na upeo wa utafiti wake.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii ina sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu fonolojia ya Kiswahili na fonolojia ya Kihaya. Sehemu ya pili inafafanua namna lugha mbalimbali ulimwenguni, barani Afrika na Tanzania zinavyoathirina. Sehemu ya mwisho inahusiana na nadharia iliyotumika katika uchanganuzi wa data ya utafiti.

#### **2.2 Maana ya Fonolojia, Fonolojia ya Kiswahili na Fonolojia ya Kihaya**

Sehemu hii imeeleza maana ya fonolojia ya lugha kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali, pia imeeleza fonolojia ya lugha ya Kiswahili na kuainisha sauti za lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa wanaisimu. Vilevile fonolojia ya Kihaya imeelezwa na kuainisha sauti za lugha ya Kihaya.

##### **2.2.1 Maana ya Fonolojia**

Kuna wataalamu mbalimbali waliotoa dhana ya fasili ya fonolojia, miongoni mwao ni Massamba na Wenzake (2001) na TUKI (1990) wanasema kuwa fonolojia ni kiwango cha sarufi kinachojishughulisha na uchambuzi wa mfumo wa sauti katika lugha.

Naye Matinde (2012) ameongeza kuwa mbali na taaluma ya fonolojia kuchunguza na kufafanua sauti za lugha, hufafanua uamilifu wa sauti hizo katika mfumo mahususi.

Kutokana na fasili za wataalam hawa tunaweza kusema kuwa fonolojia ni taaluma inayojihusisha na kuchunguza, kuchambua na kufafanua mfumo wa sauti za lugha mahususi katika lugha ya mwanadamu.



### **2.2.2 Fonolojia ya Kiswahili**

Fonolojia ya Kiswahili ni taaluma inayojihusisha na kuchunguza, kuchambua na kufafanua mfumo wa sauti za lugha ya Kiswahili. Massamba na wenzake (2012) wanasema kwamba kwa kawaida sauti za lugha zote za wanadamu hugawika katika aina kuu mbili. Aina hizo ni Irabu na konsonanti. Hivyo basi, sauti za lugha ya Kiswahili zinazoshughulikiwa na taaluma ya fonolojia ni sauti konsonanti na sauti Irabu.

### **2.2.3 Sauti Konsonanti za Kiswahili Sanifu**

Massamba na wenzake (2012) wanasema sauti konsonanti ni aina ya sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondo hewa kutoka mapafuni, ikipitia katika chemba ya kinywa na chemba ya pua kwenda nje. Mgullu (2010) na Nchimbi (2008) akimnukuu Maganga (1979, 1992:29), Batibo (1980) na TUKI (2004) wanasema kuwa zipo sauti konsonanti 25 katika lugha ya Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa Masebo na Nyangwine (2012) wanaainisha konsonanti hizo kwa kutumia vigezo vikuu vitatu.

- (i) Mahali pa kutamkia
- (ii) Namna / jinsi ya kutamka
- (iii) Mtetemo/ mtikisiko wa nyuzi sauti

#### **(A) Mahali pa Kutamkia**

Kigezo hiki huainisha konsonanti za lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia viungo katika mwili wa binadamu vinavyohusika katika utamkaji wa sauti konsonanti. Konsonanti za Kiswahili hutamkiwa katika sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na;

## (i) Midomo

Sauti hizi hutamkwa mdomo wa juu unapokutana na mdomo wa chini. Sauti konsonanti za mdomoni ni /p/, /b/, /m/ na /w/.

## (ii) Midomo na meno

Sauti hizi hutamkwa wakati mdomo wa chini unapokutana na meno ya juu. Sauti za mdomo na meno ni /f/ na /v/.

## (iii) Meno

Hutamkwa ulimi ukiwa katikati ya meno ya juu na ya chini. Ulimi hugusa meno ya juu sauti hizi zinapotamkwa. Sauti za meno ni /th/ na /dh/.

## (iv) Ufizi

Sauti hizi hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapogusana na ufizi. Sauti za ufizi ni /t/, /d/, /n/, /z/, /s/, /r/ na /l/.

## (v) Kaakaa gumu

Sauti hizi hutamkwa wakati sehemu ya kati ya ulimi inapoinuka kugusana na kaakaa gumu. Sauti za kaakaa gumu ni /ch/, /ny/, /j/, /sh/ na /y/.

## (vi) Kaakaa laini

Sauti hizi hutamkwa wakati sehemu ya nyuma ya ulimi inapoinuka kugusana na kaakaa laini. Sauti za kaakaa laini ni /k/, /g/, /ng $\emptyset$ / na /gh/.

## (vii) Koromeo/ glota

Matinde (2012) anasema glota ni uwazi uliopo kati ya nyuzi sauti zilizopo katika koromeo. Uwazi huo hubadilikabadilika katika utamkaji wa sauti mbalimbali. Sauti

hizi hutamkwa wakati koromeo limefunguliwa. Kiswahili kina sauti moja tu ya koromeo nayo ni /h/.

**(B) Namna au jinsi ya kutamka**

Kigezo hiki huonyesha jinsi hewa inavyozuiliwa na kuachiliwa wakati konsonanti zinapotamkwa. Kwa kuzingatia kigezo hiki kuna aina zifuatazo za sauti konsonanti za Kiswahili sanifu.

**(i) Vipasuo**

Katika utamkaji wa sauti hizi, hewa kutoka mapafuni husukumwa nje kwa nguvu na kuzuiliwa kabisa na kisha kuachiwa kwa ghafla na kutoa sauti ambayo hufanana na sauti isikikayo wakati kitu kinapolipuka. Kutokana na hali hiyo ya kutoa sauti ya kupasuka wanafonetiki wengi huziita sauti konsonanti hizi vipasuo. Masebo na Nyangwine (2012) wanasema kuwa vipasuo huweza kupangwa kutegemeana na mahali pa kutamkia.

- Vipasuo vya midomo

Hizi ni sauti /p/ na /b/ ambapo sauti hizi hutamkwa wakati hewa kutoka mapafuni huzuiliwa kabisa na mdomo wa chini ambao huwa umeshikana kabisa na mdomo wa juu na kisha midomo hiyo kuachia kwa ghafla na sauti hizo kutamkwa katika hali ya mlipuko.

- Vipasuo vya ufizi

Sauti hizi ni /t/ na /d/ ambapo sauti hizi hutamkwa wakati hewa kutoka mapafuni huzuiliwa kabisa na ncha ya ulimi ambayo huwa imeinuka kugusana kabisa na ufizi

na kuzuia hewa kisha ala hizo kuachia kwa ghafla na kusababisha kutoa sauti kama ya kitu kinacholipuka.

- Vipasuo vya kaaka laini

Hizi ni sauti /k/ na /g/ ambapo hewa kutoka mapafuni huzuiliwa kabisa na sehemu ya nyuma ya ulimi ambayo huwa imeinuka kugusana na kaaka laini na kisha hewa hiyo kuachiwa kwa ghafla na kutoa mlio kama wa kitu kilichopasuka.

## (ii) Vikwamizo

Sauti hizi hutamkwa wakati ambapo ala za kutamkia zinapokuwa zimekaribiana kiasi cha kutosha kuweza kusikia mkwaruzo unatokea wakati hewa inapopita kati ya ala hizo, kwa mujibu wa Masebo na Nyangwine (2012) wanasema kuwa vikwamizo pia vimepangwa katika makundi kutegemeana na mahali pa kutamkia.

- Vikwamizo vya midomo na meno

Hizi ni sauti /f/ na /v/ ambazo hutamkwa wakati mdomo wa chini unapokuwa umekaribiana kiasi cha kutosha na meno ya juu na mkwaruzo wa hewa hupita kati ya ala hizo.

- Vikwamizo vya meno

Hizi ni sauti /th/ na /dh/ ambazo hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapokuwa katikati ya meno ya juu na chini na kisha hewa kupita kwa mkwaruzo kati ya ala hizo.

- Vikwamizo vya ufizi

Hizi ni sauti /s/ na /z/ ambazo hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikiwa imeinuka kugusana na ufizi kisha hewa kupita kwa mkwaruzo kati ya ala hizo.

- Vikwamizo vya kaakaa gumu

Hii ni sauti /sh/ ambayo hutamkwa wakati sehemu ya kati ya ulimi inapoinuka kugusana na kaakaa gumu na kisha hewa kupita kwa mkwaruzo kati ya ala hizo.

- Vikwamizo vya kaakaa laini

Hii ni sauti /gh/ ambayo hutamkwa wakati sehemu ya nyuma ya ulimi inapoinuka na kugusana na kaakaa laini na hewa kupita kwa mkwaruzo kati ya ala hizo.

- Kikwamizo cha glota

Hii ni sauti /h/ ambayo hutamkiwa kwenye koromeo.

### **(iii) Vizuiwa – kwamiza/ vipasuo kwamizi**

Konsonanti hizi zinapotamkwa hewa kutoka mapafuni husukumwa nje kwa nguvu, huzuiwa halafu nafasi ndogo huachwa ili hewa ipite ikiwa na mkwaruzo. Vizuiwa kwamizwa katika Kiswahili ni /ch/ na /j/.

### **(iv) Kitambaza**

Hii ni sauti /l/ ambayo hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapogusana na ufisi na hewa nyingi hutokea pembeni mwa ulimi ambao unajisambaza kinywani kama mkeka.

### **(v) Kimadende**

Hii ni sauti /r/ ambayo hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikiwa imegusa ufizi lakini kutokana na nguvu ya hewa inayopita kati ya ncha hiyo na ufizi, ncha ya ulimi hupigapiga kwa haraka haraka kwenye ufizi.

**(vi) Ving'ong'o / nazali**

Hizi ni sauti konsonanti ambazo hutamkwa kwa kukishusha kimio kwa namna ambayo kiasi kikubwa cha hewa kutoka mapafuni huelekezwa kupita kwenye chemba ya pua. Kiswahili sanifu kinazo nazali nne, ambazo ni sauti nazali /m/, /n/, /ny/ na /ngø/. Masebo na Nyangwine (wameshatajwa) wanaendelea kusema kuwa sauti nazali /m/ hutakwa kwa midomo miwili, /n/ hutamkwa wakati ncha ya ulimi inagusana na ufizi, /ny/ hutamkwa wakati sehemu ya kati ya ulimi inapoinuka kugusana na kaakaa gumu na /ngø/ ambayo hutamkwa wakati sehemu ya nyuma ya ulimi inapoinuka kugusana na kaakaa laini.

**(vii) Viyeyusho**

Pia huitwa nusu irabu. Matinde (2012) anasema hizi ni sauti ambazo zipo katikati ya irabu na konsonanti hasa kwa misingi ya utamkaji. Wakati wa utamkaji wa viyeyusho kunakuwepo na mzuio mdogo wa mkondo hewa. Katika lugha ya Kiswahili kuna viyeyusho viwili, ambavyo ni;

- Sauti /w/ ambayo ni kiyeyusho cha midomo (hutamkwa wakati mdomo ukiwa mviringo)
- Sauti /y/ ambayo ni kiyeyusho cha kaakaa gumu (hutamkwa wakati mdomo hukiwa katika hali ya mtandazo).

**(C) Mtetemeko/mtikisiko wa nyuzi sauti**

Kwa mujibu wa kigezo hiki, kuna aina kuu mbili za sauti za Kiswahili sanifu

**(i) Sauti ghuna**

Hizi ni sauti zinapotamkwa huwa na mtetemo wa nyuzi za sauti. Sauti ghuna ni /b/, /d/, /g/, /v/, /z/, /dh/, /gh/, /j/, /l/, /r/, /m/, /n/, /ny/ na /ngø/.

## (ii) Sauti si ghuna

Hizi ni sauti ambazo zinapotamkwa huwa hamna mtikisiko wa nyuzi za sauti. Wakati mwingine huitwa sauti hafifu. Sauti hizo ni /p/, /t/, /k/, /f/, /th/, /s/, /sh/, /h/, /ch/, /w/ na /y/

**Jedwali Na. 2.1: Uainishaji wa Konsonanti kwa Kutumia Vigezo vya Uainishaji wa Konsonanti za Kiswahili Sanifu**

		midomo	Midomo meno	meno	ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	glota
Vipasuo	+ghuna	b			d		g	
	-ghuna	p			t		k	
Vikwamizo	+ghuna		v	dh	z		gh	
	-ghuna		f	th	s	sh		H
Vizuiwa kwamiza	+ghuna					j		
	-ghuna					ch		
Kitambaza	+ghuna				l			
	-ghuna							
Kimadende	+ghuna				r			
	-ghuna							
Vingøngø	+ghuna	m			n	ny	ngø	
	-ghuna							
Viyeyusho	+ghuna							
	-ghuna	w				y		

**Jedwali Na. 2.2: Sauti Konsonanti za Kiswahili Sanifu**

<b>Konsonanti</b>	<b>Herufi za Kifonetiki</b>	<b>Mfano wa neno la Kiswahili sanifu</b>
b	/b/	Babu
ch	/ /	Chana
d	/d/	Dua
dh	/ð/	Dhana
f	/f/	Fupi
g	/g/	Gogo
gh	/ /	Ghali
h	/h/	Hai
j	/ /	Jua
k	/k/	Kuku
l	/l/	Leo
m	/m/	Mia
n	/n/	Nuru
ngø	/ /	ngøa
ny	/ /	Nyoka
p	/p/	Pia
r	/r/	Rudi
s	/s/	Saa
sh	/ /	Shusha
t	/t/	Taa
th	/ /	Thamani
v	/v/	Vua
y	/y/	Yai
w	/w/	Watu
z	/z/	Zizi

Chanzo: Mtafiti Mwenyewe (2018)



### **2.2.2.1 Sauti Irabu za Kiswahili Sanifu**

Matinde (2012) anasema sauti irabu ni sauti ghuna ambayo hutamkwa bila mzuio wa hewa itokayo kwenye mapafu hadi kinywani. Wanaisimu mbalimbali akiwemo Mgullu (2010), Massamba na Wenzake (2012), Nchimbi (2008) pamoja na Matinde (2012) wameainisha aina tano za sauti irabu za Kiswahili sanifu. Matinde (2012) anadai kuwa vipo vigezo vikuu vitatu vinavyotumika kuainisha irabu za Kiswahili sanifu. Amainisha vigezo hivyo kama ifuatavyo:

- (i) Uinuko wa ulimi
- (ii) Sehemu ya ulimi
- (iii) Umbo la mdomo

#### **(A) Uinuko wa ulimi**

Ulimi huweza kuinuka ama juu kabisa, juu kiasi, au unaweza kuteremka chini kiasi au ukabaki chini kabisa. Minuko hii tofauti husababisha kupatikana aina tofauti za irabu kama ifuatavyo;

- (i) Ulimi ukiinuliwa juu sambamba na paa la kinywa tunapata ama irabu mbele yaani /i/ au irabu juu nyuma /u/
- (ii) Ulimi ukiinuliwa kati ya paa na sakafu ya kinywa, tunapata irabu za kati mbele yaani /e/ na irabu kati nyuma yaani /o/.
- (iii) Ulimi ukiwa chini sambamba na sakafu la kinywa tunapata irabu ya chini /a/

#### **(B) Sehemu ya ulimi iliyoinuka**

Kwa kawaida ulimi hugawanyika katika sehemu kuu tatu katika utamkaji wa irabu.


Sehemu hizo zipo kama ifuatavyo:

- (i) Sehemu ya mbele ikiwa sambamba na ufizi, irabu huainishwa kuwa ya mbele. Katika lugha ya Kiswahili irabu ya mbele ni /i/ na /e/
- (ii) Sehemu ya nyuma ikiwa sambamba na kaaka laini, irabu huainishwa kuwa ya nyuma. Katika lugha ya Kiswahili sanifu irabu ya nyuma ni /o/ na /u/.
- (iii) Sehemu ya kati ya ulimi ikiwa sambamba na kaaka gumu, irabu huainishwa kuwa irabu ya chini. Katika lugha ya Kiswahili sanifu irabu ya chini ni /a/.

**(C) Umbo la mdomo**

Wakati wa kutamka irabu za kiswahili sanifu, sura ya midomo inaweza kuwa ama mviringo au mtandazo. Sura hizi mbili tofauti za midomo husababisha kupatikana aina tofauti za irabu;

- (i) Midomo mviringo, sura ya midomo ikiwa mviringo wakati wa kutamka irabu, irabu zifuatazo huweza kuainishwa. Irabu hizo ni /o/ na /u/
- (ii) Midomo mtandazo, sura ya midomo ikiwa mtandazo, hutusaidia kuainisha irabu /i/, /e/ na /a/.



**Kielelezo Na. 2.1: Kielelezo cha Kuonyesha Ulimi Wakati wa Utamkaji wa Irabu**

**Jedwali Na. 2.3: Sauti Irabu za Kiswahili Sanifu**

<b>Irabu</b>	<b>Maandishi ya kifonetiki</b>	<b>Mfano wa neno la kiswahili</b>
i	/i/	Imba
e	/e/	Embe
a	/a/	Kaa
o	/ /	Okoa
u	/u/	Ua

Chanzo: Mtafiti mwenyewe (2018)

**2.2.3 Fonolojia ya Kihaya**

Fonolojia ya Kihaya ni taaluma inayojishughulisha na kuchunguza, kuchambua na kufafanua sauti za lugha ya Kihaya. Kwa mujibu wa Chully (2017) sauti za lugha ya Kihaya zimegawanyika katika makundi makuu mawili, ambayo ni sauti konsonanti na sauti irabu.

**2.2.3.1 Sauti Konsonanti za Lugha ya Kihaya**

Chully (2017) anataja kuwa sauti konsonanti za lugha ya Kihaya ni 20 ambazo nazo huainishwa kwa kutumia vigezo vikuu vitatu. Vigezo hivyo vipo kama ifuatavyo;

- (i) Mahali pa kutamkia
- (ii) Namna / jinsi ya kutamka
- (iii) Mtetemo / mtikisiko wa nyuzi za sauti

**(A) Mahali pa kutamkia**

Kigezo huangalia viungo katika kinywa cha binadamu vinavyohusika na utamkaji wa sauti. Viungo vinavyohusika na utamkaji pamoja za sauti zake vipo kama ifuatavyo;

## (i) Midomo

Hizi ni sauti ambazo hutamkwa wakati mdomo wa juu unapokutana na mdomo wa chini. Sauti hizo ni /p/, /b/, /m/ na /w/.

## (ii) Midomo na meno

Sauti hii utamkwa wakati mdomo wa chini unapokutana na meno ya juu. Sauti hiyo ni /f/

## (iii) Ufizi

Sauti hizi hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapoinuka kugusana na ufizi. Sauti za ufizi ni /t/, /d/, /n/, /z/, /s/, /r/ na /l/.

## (iv) Kaakaa gumu

Sauti hizi hutamkwa wakati sehemu ya kati ya ulimi inapoinuka kugusana na kaakaa gumu. Sauti za kaakaa gumu ni /ch/, /ny/, /j/, /sh/ na /y/.

## (v) Kaakaa laini

Sauti hizi hutamkwa wakati sehemu ya nyuma ya ulimi inapoinuka kugusana na kaakaa laini. Sauti za kaakaa laini ni /k/ na /g/.

## (vi) Glota/ koromeo

Hutamkwa wakati koromeo limefunguliwa. Katika lugha ya Kihaya sauti ya glota ni /h/.

Kwa mujibu wa kigezo cha mahali pa kutamkia kuna utofauti mkubwa kati ya sauti za Kihaya na sauti za lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kihaya haina sauti zinazotamkiwa kwenye meno ambazo ni sauti /dh/ na /th/. Vile vile lugha ya Kihaya ina sauti midomo na meno moja tu ambayo ni /f/ wakati katika lugha ya Kiswahili sauti zinazotamkiwa

kwenye midomo na meno ni mbili ambazo ni sauti /f/ na /v/, hivyo lugha ya Kihaya haina sauti /v/. Pia lugha ya Kihaya ina sauti za kaakaa laini mbili tu ambazo ni /k/ na /g/ wakati lugha ya kiswahili ina sauti nne zinazotamkiwa kwenye kaakaa laini ambazo ni /k/, /g/, /ng∅/ na /gh/, hivyo lugha ya Kihaya haina sauti /ng∅/ na /gh/.

Richard na Sampson (1974) wanasema kuwa mwanafunzi hutamka sauti za lugha mpya kwa kuzingatia sauti za lugha yake ya kwanza. Hivyo kutokana na baadhi ya sauti kutokuwemo katika mfumo wa mahali pa kutamkia katika lugha ya Kihaya lakini zimo katika mfumo wa mahali pa kutamkia katika lugha ya Kiswahili lazima mwanafunzi anayejifunza Kiswahili afanye makosa ya kimatamshi na kimaandishi wakati wa kujifunza sauti za Kiswahili sanifu. Hivyo utofauti huu ulimwongoza mtafiti kupitia kwa makini kazi andishi za wanafunzi ili kuweza kutambua makosa ya kifonolojia na chanzo cha makosa hayo.

### **(B) Namna au jinsi ya kutamka**

Kigezo hiki huangalia namna hewa inavyozuiliwa na kuachiliwa wakati wa kutamka konsonanti za lugha ya Kihaya. Kutokana na kigezo hiki tunapata aina zifuatazo za konsonanti:

#### **(i) Vipasuo**

Katika utamkaji wa sauti hizi, hewa kutoka mapafuni husukumwa nje kwa nguvu na kuzuiliwa kabisa na kisha kuachiwa kwa ghafla na kutoa sauti ambayo hufanana na sauti isikikayo wakati kitu kinapolipuka. Vipasuo vya lugha ya Kihaya ni /p/, /b/, /t/, /d/, /k/ na /g/. Hivyo, kwenye vipasuo vya lugha ya Kihaya na vile vya lugha ya Kiswahili hakuna utofauti wowote.

## (ii) Vikwamizo

Sauti hizi hutamkwa wakati ambapo ala za kutamkia zinapokuwa zimekaribiana kiasi cha kutosha kuweza kusikia mkwaruzo unatokea wakati hewa inapopita kati ya ala hizo. Vikwamizo vilivyo katika lugha ya Kihaya ni /f/, /s/, /z/, /sh/ na /h/. Ukichunguza vikwamizo vya lugha ya Kihaya na vile vya Kiswahili sanifu utaona utofauti mkubwa sana ambapo katika lugha ya Kihaya hakuna vikwamizo /v/, /th/, /dh/ na /gh/. Utofauti huu huweza kusababisha makosa ya kifonolojia kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

## (iii) Vizuiwa ó kwamiza

Konsonanti hizi za lugha ya Kihaya hutamkwa huku hewa ikisukumwa nje kwa nguvu, huzuiwa halafu nafasi ndogo huachwa ili hewa ipite ikiwa na mkwaruzo. Vizuiwa kwamiza vya lugha ya Kihaya ni /ch/ na /j/. Vizuiwa kwamiza vya lugha ya Kihaya na vile vya lugha ya Kiswahili havina utofauti wowote.

## (iv) Kitambaza

Hii ni sauti /l/ ambayo hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapogusana na ufisi na hewa nyingi hutokea pembeni mwa ulimi ambao unajisambaza kinywani kama mkeka.

## (v) Kimadende

Hii ni sauti /r/ ambayo hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikiwa imegusa ufizi lakini kutokana na nguvu ya hewa inayopita kati ya ncha hiyo na ufizi, ncha ya ulimi hupigapiga kwa haraka haraka kwenye ufizi.

## (vi) Vingøngø / nazali

Hizi ni sauti konsonanti ambazo hutamkwa kwa kukishusha kimio kwa namna ambayo kiasi kikubwa cha hewa kutoka mapafuni huelekezwa kupita kwenye chemba ya pua. Lugha ya Kihaya inazo nazali tatu tu, ambazo ni sauti nazali /m/, /n/ na /ny/. Katika lugha ya Kihaya nazali /ngø/ haipo lakini katika lugha ya Kiswahili sauti /ngø/ ipo.

Hivyo ukosefu wa sauti hiyo katika lugha ya Kihaya yaweza kuwa moja ya sababu zinazosababisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

## (vii) Viyeyusho

Hizi ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka hewa haizuiliwi mahali popote. Sauti hizo ni /w/ na /y/.

**C Mtetemeko/mtikisiko wa nyuzi sauti**

Kwa mujibu wa kigezo hiki, kuna aina kuu mbili za sauti za Kiswahili sanifu.

## (i) Sauti ghuna

Hizi ni sauti zinapotamkwa huwa na mtetemo wa nyuzi za sauti. Sauti ghuna ni /b/, /d/, /g/, /z/, /j/, /l/, /r/, /m/, /n/ na /ny/.

## (ii) Sauti si ghuna

Hizi ni sauti ambazo zinapotamkwa huwa hamna mtikisiko wa nyuzi za sauti. Wakati mwingine huitwa sauti hafifu. Sauti hizo ni /p/, /t/, /k/, /f/, /s/, /sh/, /h/, /ch/, /w/ na /y/

**Jedwali Na. 2.4: Uainishaji wa Konsonanti kwa Kutumia Vigezo vya Uainishaji wa Konsonanti za Lugha ya Kihaya**

		midomo	Midomo meno	ufizi	Kaaka gumu	Kaaka laini	Glota
Vipasuo	+ghuna	b		d		g	
	-ghuna	p		t		k	
Vikwamizo	+ghuna			z			
	-ghuna		f	s	sh		H
Vizuiwa kwamiza	+ghuna				j		
	-ghuna				ch		
Kitambaza	+ghuna			l			
	-ghuna						
Kimadende	+ghuna			r			
	-ghuna						
Ving'ong'o	+ghuna	m		n	ny		
	-ghuna						
Viyeyusho	+ghuna						
	-ghuna	w			y		

Chanzo: Mtafiti mwenyewe (2018)

**Jedwali Na. 2.5: Sauti Konsonanti za Kihaya**

Konsonanti za Kihaya	Maandishi Kifonetiki	Mfano wa neno kwa Kihaya	Tafsiri ya neno kwa Kiswahili
p	/p/	mpola	Pole
b	/b/	binga	Fukuza
t	/t/	tema	Kata
d	/d/	enda	Vunja
k	/k/	kifuba	Kifua
g	/g/	gamba	Sema
f	/f/	fundikila	Funika
s	/s/	singa	Sugua
z	/z/	zana	Cheza
sh	/ /	sheka	Cheka
ch	/ /	chumba	Pika
l	/l/	leba	Angalia
r	/r/	rola	Hai
ny	/ /	nyegera	Karibu
n	/n/	nagira	Sinzia
m	/m/	mata	Maziwa
h	/h/	huririza	Sikiliza
j	/ /	juna	Saidia
y	/y/	yombeka	Jenga
w	/w/	waitu	Kwetu

Chanzo: Chully (2017) imeboreshwa na Mtafiti (2018)



### **2.2.3.2 Sauti Irabu za Lugha ya Kihaya**

Lugha ya Kihaya ina sauti irabu tano (5) tu. Uainishaji wa sauti irabu za lugha ya Kihaya huzingatia vigezo vile vile vinavyotumika katika lugha ya Kiswahili. Sauti irabu za lugha ya Kihaya za zile za lugha ya Kiswahili hazina utofauti wowote kutokana na idadi ya irabu zenyewe, mwinuko wa ulimi, sehemu ya ulimi na umbo la mdomo wakati wa kutamka irabu hizo katika lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili. Vigezo vinavyotumika kuainisha irabu za lugha ya Kihaya ni hivi vifuatavyo;

- (i) Mwinuko wa ulimi
- (ii) Sehemu ya ulimi iliyoinuka
- (iii) Umbo la mdomo.

#### **(A) Uinuko wa ulimi**

Ulimi huweza kuinuka ama juu kabisa, juu kiasi, au unaweza kuteremka chini kiasi au ukabaki chini kabisa. Minuko hii tofauti husababisha kupatikana aina tofauti za irabu kama ifuatavyo:

- (i) Ulimi ukiinuliwa juu sambamba na paa la kinywa tunapata ama irabu mbele yaani /i/ au irabu juu nyuma /u/
- (ii) Ulimi ukiinuliwa kati ya paa na sakafu ya kinywa, tunapata irabu za kati mbele yaani /e/ na irabu kati nyuma yaani /o/.
- (iii) Ulimi ukiwa chini sambamba na sakafu la kinywa tunapata irabu ya chini /a/

#### **(B) Sehemu ya ulimi iliyoinuka**

Kwa kawaida ulimi hugawanyika katika sehemu kuu tatu katika utamkaji wa irabu.

Sehemu hizo zipo kama ifuatavyo:

- (i) Sehemu ya mbele ikiwa sambamba na ufizi, irabu huainishwa kuwa ya mbele. Katika lugha ya Kihaya irabu ya mbele ni /i/ na /e/
- (ii) Sehemu ya nyuma ikiwa sambamba na kaaka laini, irabu huainishwa kuwa ya nyuma. Katika lugha ya Kihaya sanifu irabu ya nyuma ni /o/ na /u/.
- (iii) Sehemu ya kati ya ulimi ikiwa sambamba na kaaka gumu, irabu huainishwa kuwa irabu ya chini. Katika lugha ya Kihaya sanifu irabu ya chini ni /a/.

**(C) Umbo la mdomo**

Wakati wa kutamka irabu za Kihaya, sura ya midomo inaweza kuwa ama mviringo au mtandazo. Sura hizi mbili tofauti za midomo husababisha kupatikana aina tofauti za irabu;

- (i) Midomo mviringo, sura ya midomo ikiwa mviringo wakati wa kutamka irabu, irabu zifuatazo huweza kuainishwa. Irabu hizo ni /o/ na /u/
- (ii) Midomo mtandazo, sura ya midomo ikiwa mtandazo, hutusaidia kuainisha irabu /i/, /e/ na /a/.

**Jedwali Na. 2.6: Sauti Irabu za Kihaya**

<b>Irabu ya Kihaya</b>	<b>Maandishi Kifonetiki</b>	<b>Mfano wa neno katika Kihaya</b>	<b>Tafsiri ya neno katika Kiswahili</b>
i	/i/	imuka	Amka
e	//	ente	ngøombe
a	/a/	akala	Kidole
o	//	oburola	Uhai
u	/u/	uguruka	Kuruka

Chanzo: Chully (2017) Imeboreshwa na Mtafiti (2018)

Hivyo basi, zipo sauti konsonanti ambazo zipo katika lugha ya Kiswahili sanifu lakini hazipo katika lugha ya Kihaya. Sauti konsonanti ambazo zipo katika lugha ya Kiswahili sanifu ila hazipo katika lugha ya Kihaya ni sauti /dh/, /gh/, /ngø/, /th/ na /v/. Tofauti katika sauti konsonanti za Kiswahili sanifu na lugha ya Kihaya yaweza kuwa moja ya sababu ya makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

#### **2.2.4 Silabi**

Kwa mujibu wa Matinde (2012) anasema silabi ni dhana ya kimofolojia ambayo huwakilisha umbo la matamshi ambapo sauti moja au zaidi hutamkwa kwa mara moja kama fungu moja. Kwa hiyo, silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho ni kikubwa kuliko fonimu lakini kidogo kuliko neno katika mfumo wa kidarajia. Silabi huundwa na fonimu moja au zaidi. Kila lugha huwa na miundo yake ya silabi. Kuna uwezekano mkubwa kukawepo na miundo tofauti kati ya silabi za lugha ya Kihaya na za lugha ya Kiswahili na kupelekea makosa ya kifonolojia miongoni mwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Katika tasnifu hii ya utafiti ishara # itatumika kuonyesha mipaka ya maneno na ishara \$ itatumika kuonyesha mipaka ya silabi.

##### **2.2.4.1 Miundo ya Silabi za Kiswahili Sanifu**

Mgullu (2010) anasema lugha ya Kiswahili inayo miundo ya silabi ipatayo saba, nayo ni:

##### **(i) Silabi za konsonanti + irabu (KI)**

Katika lugha ya Kiswahili muundo huu unatumika kuliko miundo mingine yote ambapo silabi huundwa na mfuatano wa konsonanti na irabu.

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>
Mama	#ma\$ma#
Kitabu	#ki\$ta\$bu#
Samaki	#sa\$ma\$ki#

**(ii) Silabi za irabu (I)**

Silabi za irabu huwa na irabu peke yake ambayo huwa ni silabi. Kiswahili kinazo silabi nyingi za irabu.

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>
ua	#u\$a#
uasi	#u\$a\$si#
adi	#a\$du\$i#

**(iii) Silabi za konsonanti (K)**

Katika lugha ya Kiswahili, konsonanti ambazo zinaweza kuwa silabi katika lugha ya Kiswahili ni zile za aina ya nazali tu. Konsonanti hizo hasa ni mbili: nazali /m/ na /n/. Konsonanti hizi zinakuwa silabi katika mazingira maalumu au maneno maalumu. Si lazima ziwe silabi kila wakati zinapotumika (Mgullu, 2010).

<b>Neno</b>	<b>Silabi</b>
Mpaka	#m\$pa\$ka#
Mtu	#m\$tu#
Nchi	#n\$chi#
Nta	#n\$ta#

**(iv) Silabi za konsonanti + konsonanti + irabu (KKI)**

Muundo huu wa silabi huwa na mfuatano wa konsonanti, konsonanti na irabu ili kuunda silabi ya neno la Kiswahili.

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>
Penda	#pe\$nda\$
Unga	#u\$nga#
Mbegu	#mbe\$gu#

**(v) Silabi za konsonanti + kiyeyusho + Irabu**

Hizi ni silabi zenye konsonanti, kiyeyusho /w/ au /y/ pamoja na irabu. Maneno katika lugha ya Kiswahili yenye muundo huo wa silabi yapo kama ifuatavyo;

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>
Afya	#a\$fya#
Mwanga	#mwa\$nga#
Pweza	#pwe\$za#

**(vi) Silabi za konsonanti + konsonanti + kiyeyusho + irabu**

Lugha ya Kiswahili ina maneno machache sana yenye silabi ambazo zina muundo wa konsonanti, konsonanti, kiyeyusho na irabu.

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>
Mbweha	#mbwe\$ha#
Jangwa	#ja\$ngwa#
Ngwara	#ngwa\$ra#

**(vii) Silabi funge**

Matinde (2012) anasema silabi funge ni zile silabi ambazo huishia kwa konsonanti. Maneno mengi yenye silabi funge katika lugha ya Kiswahili ni yale maneno yaliyokopwa kutoka lugha nyingine za kigeni kama vile Kiarabu au Kiingereza na kuingizwa katika lugha ya Kiswahili.

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>
Daftari	#daf\$ta\$ri#
Labda	#lab\$da#
Daktari	#dak\$ta\$ri#

**2.2.4.2 Muundo wa Silabi za Lugha ya Kihaya**

Silabi za lugha ya Kihaya zina miundo yake tofauti na zile silabi za maneno ya Kiswahili. Hii ni kutokana na utaratibu wa kila lugha kuwa muundo wake na utaratibu wake wa uundaji wa maneno. Silabi hizo za lugha ya Kihaya zina muundo ufuatao:

**(i) Muundo wa irabu pekee**

Yapo baadhi ya maneno katika lugha ya Kihaya ambayo irabu huweza kusimama pekee yake na kuhesabiwa kama silabi.

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>	<b>Kiswahili chake</b>
Eibanga	#e\$i\$ba\$nga#	mlima
Zaitu	#za\$i\$tu#	zetu
Abana	#a\$ba\$na#	watoto

**(ii) Muundo wa konsonanti + irabu**

Silabi nyingi za lugha ya Kihaya zina muundo huu wa konsonanti na irabu.

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>	<b>Kiswahili chake</b>
Omutima	#o\$mu\$ti\$ma#	moyo
Mushemererwe	#mu\$she\$me\$re\$uwe#	mfurahie
Kusima	#ku\$si\$ma#	kushukuru

**(iii) Muundo wa konsonanti + konsonanti+ irabu**

Muundo huu hujumuisha konsonanti inayofatiwa na konsonanti ya nazali /m/ au /n/ au kiyeyusho /w/ au /y/ pamoja na irabu. Mifano ya maneno yenye muundo huo wa silabi kutoka katika lugha ya Kihaya upo kama ifuatavyo;

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>	<b>Kiswahili chake</b>
Byange	#bya\$nge#	vyangu
Ndinda	#ndi\$nda#	nisubirie
Mberwe	#mbe\$uwe#	nibarikiwe

**(iv) Muundo wa konsonanti + konsonanti + kiyeyusho+ irabu**

Silabi zenye muundo huu katika lugha ya Kihaya ni chache sana.

<b>Neno</b>	<b>silabi</b>	<b>Kiswahili chake</b>
Shangwaho	#sha\$ngwa\$ho#	kukutwa
Mbwega	#mbwe\$ga#	kujifunza

Kwa kuangalia muundo wa silabi za lugha ya Kihaya na silabi za lugha ya Kiswahili, unaona uwepo wa tofauti kubwa katika miundo ya silabi za lugha hizo mbili. Kwanza kabisa lugha ya Kihaya inaonekana kutokuwa na silabi za konsonanti pekee kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Vile vile lugha ya Kihaya inaonekana kutokuwa na silabi funge ambazo zinapatikana katika maneno ya Kiswahili sanifu. Hivyo hali hii

ilimsaidia mtafiti kuchunguza maneno ya Kiswahili sanifu yenye silabi za konsonanti pekee na silabi funge ili kubaini kama kuna makosa yoyote ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

### **2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Ujifunzaji wa Lugha na Uhusiano Wake wa Kuathiriana**

Ufundishaji wa lugha ulimwenguni una historia ndefu sana. Suala la ufundishaji lugha lilianza kutiliwa mkazo katika nchi za Magharibi mapema katika karne ya 14 wakati Kilatini kilipokuwa lugha pekee ya matumizi katika shughuli za biashara, elimu, dini na utawala. Katika karne ya 16, lugha ya Kiingereza, Kifaransa, na Kiitaliano zilianza kutambuliwa kutokana na mabadiliko ya Kisiasa (Richard na Rodgers 1986).

Njeru (2013) anasema katika bara la Afrika, kabla ya ukoloni kila kabila lilikuwa na lugha yake ambayo waliitumia kama lugha mama (lugha ya kwanza). Wakati wa ukoloni makabila tofauti yaliunganishwa na kuunda nchi moja ambapo kila kabila liliongea lugha yake. Kutokana na mwingiliano wa makabila tofauti iliwalizimu watu hao kujifunza lugha nyingine tofauti na lugha zao za kwanza. Njeru anasema kuwa lugha ya Kiingereza imekuwa lugha ya pili ya watu wengi tangu katikati mwa karne ya 19 kwenda karne ya 20. Anaendelea kusesitiza kuwa lugha ya pili kwa sasa watu wengi hujifunza kupitia shuleni na taasisi nyingine za kijamii. Njeru alitafiti athari za lugha za kibantu nchini Kenya zinavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wa shule za msingi. Katika utafiti wake alibaini kuwa lugha za kibantu nchini Kenya huathiri matamshi, tahajia na sarufi ya lugha ya Kiingereza hasa wanafunzi wa shule za msingi ambao hujifunza lugha ya Kiingereza. Aidha,



amebainisha kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili huambatana na mambo mengi kisarufi ikiwemo ujifunzaji wa miundo ya maneno, matamshi ya maneno, maumbo ya maneno, na maana za maneno. Ujifunzaji wa sarufi ya lugha ya pili ndiyo husababisha kuathiriwa kwake na lugha ya kwanza. Kazi ya Njeru ilimsaidia mtafiti kusoma kwa makini kazi andishi za wanafunzi ili kubaini utofauti wa miundo ya silabi za lugha ya Kihaya na za Kiswahili zinaweza kusababisha makosa ya kifonolojia kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Corder (1967) anasema watu hujifunza lugha ya pili huku wakiwa na lugha ya kwanza. Kwa hiyo humudu sheria na kanuni za lugha ya kwanza kujifunza na kuelewa lugha ya pili. Anaendelea kusesitiza kuwa matumizi ya sheria hizo za lugha ya kujifunza lugha ya pili ndiyo hupelekea watu kufanya makosa wakati wa kuzungumza au kuandika lugha ya pili. Makosa hayo huweza kuwa ya kimatamshi, kitahajia, au ya kisarufi. Kazi hii ya Corder ilimsaidia mtafiti kujua mbinu zipi zitumike katika kuwasaidia wanafunzi wanaozungumza Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Tremblay (2017) anasema kuwa suala la matamshi katika lugha ya kwanza ndilo hutawala zaidi matamshi ya sauti za maneno katika lugha ya pili. Tremblay anaendelea kusesitiza kuwa pamoja na kuwepo muda wa kujifunza lugha, suala la matamshi katika lugha mama ni la kiasili, hivyo huchukua muda kuweza kubadilika. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kujua ni kipi kinasababisha wanafunzi wanaozungumza Kihaya kufanya makosa ya kifonolojia wakati wa kujifunza Kiswahili sanifu. Pia ilimsaidia kujua mbinu za kutumia ili kuepuka makosa haya.

Mudhune (1994) alichunguza ujifunzaji wa mofosintaksia ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Kiluo kwa mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi. Anadai kuwa makosa kadhaa yaliyojitokeza katika kazi za wanafunzi husika yalitokana na athari za lugha yao ya kwanza (Kiluo). Hata hivyo, alisisitiza kuwa kulikuwa na makosa mengine yaliyogunduliwa na ambayo hayakuwa na chanzo chake katika lugha ya kwanza iliyotumiwa na wanafunzi waliochunguzwa. Kazi hii ya utafiti, ilimsaidia mtafiti kutambua kuwa kuna makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu lakini makosa hayo hayatokani au hayasababishwi na Kihaya kama lugha ya kwanza ya Wahaya.

Kwa upande wake, Massamba (1986) katika kuchunguza athari za lugha mama (lugha za kienyeji) katika Kiswahili mkoani Mara nchini Tanzania, aligundua kuwa lugha za kienyeji na lugha ya Kiswahili ziliathiriana. Alichunguza jinsi lugha za kienyeji zilivyokiathiri Kiswahili katika viwango mbalimbali. Anaeleza kwamba, lugha za kienyeji katika mkoa wa Mara zilikiathiri Kiswahili kifonolojia, kimsamiati na kisarufi. Katika fonolojia, Massamba anaonesha jinsi sauti zilivyoongezwa au kudondoshwa katika matumizi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha za kwanza, hali iliyosababisha makosa ya utamkaji. Kwa mfano baadhi ya lugha za Kienyeji huongeza sauti /u/ katika neno **mtu** na kuwa **mutu**, vile vile udondosha sauti /h/ katika baadhi ya maneno. Katika neno **habari** sauti /h/ udondoshwa neno hilo uandikwa **abari**. Utafiti huu ulimwongoza mtafiti kubainisha kama makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu hutokana na uchopekaji wa vitamkwa au udondoshaji wa vitamkwa wakati wa kuzungumza kiswahili sanifu.

Aidha, Nyanda (2015) alifanya utafiti kuchunguza athari za lugha ya Kinyamwezi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Katika utafiti wake alibainisha athari za kimatamshi, kimsamiati na kimaana ambazo zinatokana na Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Nyanda anaonyesha kuwa katika athari za kimatamshi Wanyamwezi huchanganya sauti /r/ na /l/, pia wameathirika katika matumizi ya sauti /gh/, /th/, /dh/ na /b/. sauti hizo hazipo katika lugha ya Kinyamwezi. Hivyo wanafunzi wengi hupata shida kuzitamka wakati wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Vile vile mtafiti alibainisha kuwa Wanyamwezi wana tabia ya kuchopeka sauti katika neno wakati wa kuongea lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, wanyamwezi wanasema ònilikwendaga badala ya nilikwendaö, õhaimbagi badala ya haimbiö.

Hivyo kiambisha {g} huambikwa baada ya mzizi wa neno la Kiswahili na kuathiri matamshi ya neno husika. Pia alibainisha kuwa Wanyamwezi wana tabia ya kudondosha baadhi ya sauti wakati wa kutamka maneno ya Kiswahili ambapo /h/ hudondoshwa mara kwa mara. Kwa mfano hutamka arusi badala ya harus. Hivyo, Kazi hii ilimsaidia mtafiti kubainisha kama makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili sanifu yanasababishwa Kihaya kutokuwa na baadhi ya vitamkwa lakini vitamkwa hivyo vipo katika lugha ya Kiswahili sanifu. Vilevile ilimsaidia mtafiti kubainisha kama wazungumzaji wa Kihaya wana uchopekaji au udondoshaji wa baadhi ya vitamkwa wakati wa kuzungumza au kuandika Kiswahili sanifu.

Wenceslaus (2015) naye alifanya uchunguzi wake juu ya athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Katika uchunguzi wake alibainisha athari za kifonolojia za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya pili ambayo ni Kiswahili.

Wenceslaus (ameshatajwa) anaeleza kuwa kifonolojia kuna mwingiliano mkubwa wa sauti za lugha ya Kijita na lugha ya Kiswahili ambapo baadhi ya Wajita hutamka kwa makosa baadhi ya sauti za lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, Wajita hutamka /z/ badala ya /dh/, katika neno “**dharau**” husema “**zarau**”. Pia kazi hii ilimsaidia mtafiti kubainisha vitamkwa vilivyo katika lugha Kiswahili lakini havipo katika lugha ya Kihaya na kuonyesha namna wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili wanavyotamka vitamkwa hivyo.

#### **2.4 Nadharia ya Utafiti**

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni Uchanganuzi Makosa. Nadharia hii hutumia mbinu za kiisimu katika kuangazia makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha. Uchanganuzi Makosa ni nadharia inayochunguza makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha ya pili (Gas na Selinker, 2008). Mtazamo huu huzingatia ulinganishi wa makosa yanayojitokeza katika matumizi ya lugha lengwa kwa kujikita humo humo katika lugha lengwa husika. Mwasisi wa nadharia hii ni Corder (1967), ambaye kupitia makala ya “The Significance of Learners’ Errors”, nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilichukua mwelekeo mpya.

Kwa mujibu wa Keshavarz (2012), kihistoria suala la uchunguzi wa lugha ulianza katika karne ya 18 ambapo wataalamu mbalimbali wa lugha walianza kulinganisha lugha mbalimbali ili kuonyesha uhusiano na ufanano wa lugha ulimwenguni. Nadharia waliyoitumia wataalamu hao ni nadharia ya Uchanganuzi Linganishi (contrastive analysis). Kazi kubwa ya nadharia hii ilikuwa ni kuchambua tofauti na ufanano wa kimuundo wa makundi mbalimbali ya lugha ili kueleza ni kwa nini sifa za lugha fulani ni ngumu kujifunza kulinganisha na lugha nyingine. Hivyo nadharia ya

uchanganuzi linganishi ilitoa orodha ya ufanano na utofauti wa Kiisimu baina ya lugha mbili zilizokuwa zinalinganishwa au kutofautishwa. Khalfan (2011) anasema kuwa nadharia ya uchanganuzi linganishi ilikuwa na mitazamo mitatu, ambayo ni:

- (i) Kutengeneza kanuni na taratibu za kiisimu za aina moja ambazo zingeliongoza lugha zote ulimwenguni.
- (ii) Kueleza na kutabiri makosa yanayoweza kujitokeza katika kujifunza lugha ya pili.
- (iii) Kuanzisha vifaa na mbinu za kufundishia lugha.

Hivyo, nadharia ya uchanganuzi linganishi ilionekana kuwa na udhaifu mkubwa sana katika uchambuzi wa makosa katika lugha. Moja ya udhaifu wake ni kuwa si kila aina ya makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha huweza kutabiriwa. Vile vile makosa katika matumizi ya lugha yalichukuliwa kama kasoro ambazo zilitakiwa kuondolewa kabisa.

Kutokana na udhaifu wa nadharia ya uchanganuzi linganishi katika uchambuzi wa makosa katika ujifunzaji wa lugha, kuliibuka nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Corder (1967) alisisitiza kuwa makosa husika yalikuwa muhimu kwa mwanafunzi kwa kuwa yaliweza kuchukuliwa kama kifaa alichotumia katika ujifunzaji wake. Gass na Selinker (1994) walielezea makosa kama ishara wazi zilizodhihirisha ujuzi wa mwanafunzi katika lugha ya pili. Kwa upande mwingine, makosa hutumiwa na mtafiti katika juhudi za kugundua mikakati itumiwayo na watu katika upataji wa lugha (Richards, 1974; Taylor, 1975; Dulay na Burt, 1974). Makosa yalianza kuchukuliwa kama elementi za utafiti wa kiisimu ambazo zilikuwa zimepuuzwa kwa kipindi kirefu.

Aidha, makosa yalionwa kama mifumo ya kiisimu ambayo ilitumiwa na wanafunzi katika mawasiliano na ujifunzaji wa lugha lengwa. Corder (1967) alizungumza umuhimu wa makosa ya wanafunzi katika matumizi ya lugha. Kulingana na Corder, misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ni kama ifuatayo:

- (i) Katika ujifunzaji wa L2, mwanafunzi lazima afanye makosa.
- (ii) Kufanya makosa ni kawaida kwa hivyo mwanafunzi anapofanya makosa asiadhibiwe bali makosa hayo yachukuliwe kama kigezo cha kuthibitisha kuwa mwanafunzi bado hajajifundisha lugha.

Corder (1973) anasema kuwa zipo hatua kuu tatu za uchanganuzi makosa katika lugha, ambazo zimefafanuliwa kama ifuatavyo:

- (i) Utambuzi wa makosa

Hii ni hatua ya kwanza katika utambuzi wa makosa katika lugha. Katika hatua hii mtafiti anasoma maneno aliyoandika mwanafunzi na kuamua iwapo maneno hayo yana makosa au la. Makosa yanaweza kutambuliwa kwa kufanya ulinganisho kati ya kanuni za lugha ya pili (anayojifunza) na lugha ya kwanza ya mwanafunzi. Hivyo katika utafiti huu, mtafiti alisoma kwa umakini kazi mbalimbali zilizofanywa na wanafunzi katika madaftari yao na kuweza kutambua makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

- (ii) Uchambuzi wa makosa

Katika hatua hii makosa huelezwa kwa misingi ya ulinganisho. Makosa yaliyoonekana kujirudia rudia kwa mwanafunzi uchambuliwa kama makosa na kuonyesha ni kipi alichotaka kusema kutokana na taratibu za lugha lengwa. Mtafiti

katika utafiti huu alichambua makosa yaliyokuwa yanajirudia rudia katika kazi za mwanafunzi na kuyaandika katika shajara lake ili kutumia makosa hayo katika uchambuzi na uchanganuzi wa data yake. Kosa lililojitokeza mara moja halikuchukuliwa kama kosa.

(iii) Ufafanuzi wa makosa

Katika hatua hii mtafiti hueleza ni kwa nini na jinsi gani makosa hutokea. Mtafiti hueleza ni aina gani ya kosa mwanafunzi amefanya na kwa nini amefanya. Makosa yanayochambuliwa katika lugha huweza kuwa katika aina kuu tatu, ambazo ni;

- (i) Makosa ya uhamisho- Haya ni makosa ya yanayosababishwa na lugha ya kwanza kuingiliana na lugha ya pili.
- (ii) Makosa ya ulinganisho ó Haya ni makosa yanayosababishwa na mwanafunzi mwenyewe.
- (iii) Makosa ya ufundishaji ó makosa haya husababishwa na vifaa na mbinu za ufundishaji wa lugha.

Hivyo, mtafiti katika utafiti huu, alifafanua aina ya makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu na kueleza kwa nini wamefanya makosa hayo na sababu za uwepo wa makosa hayo pamoja na kupendekeza mbinu za kutumia ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili.

## **2.5 Muhtasari**

Sura hii ya pili imejadili kwa kina mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia. Katika mapitio ya kazi tangulizi, mtafiti amefafanua maana ya fonolojia, fonolojia ya

Kiswahili na fonolojia ya Kihaya. Vile vile mtafiti ameweka wazi nadharia aliyoitumia katika uchambuzi wa data. Nadharia iliyotumika ni Uchanganuzi wa Makosa.



## **SURA YA TATU**

### **MBINU NA NJIA ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii ina vipengele vikuu saba. Vipengele hivyo ni aina ya utafiti ambao mtafiti ameufanya, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, njia za kukusanyia data, vifaa vya kukusanyia data, uchambuzi wa data na muhtasari wa sura hii.

#### **3.2 Aina ya Utafiti**

Utafiti huu ni utafiti wa uwandani. Katika aina hii ya utafiti mtafiti alikutana na wasailiwa kwa kufanya nao mahojiano ya ana kwa ana pamoja na kuwapatia hojaji kwa lengo la kukusanya data ili kuweza kubainisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa lugha ya Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Katika utafiti huu wa uwandani mtafiti alikutana na wanafunzi wa shule za msingi wa darasa la tatu na darasa la nne, walimu wao pamoja na baadhi ya wazazi wenye uwezo wa kuzungumza Kihaya na Kiswahili sanifu. Pia katika utafiti huu wa uwandani mtafiti alifanya usomaji makini kwa kupitia kazi andishi za wanafunzi kwa lengo la kuchambua makosa ya kifonolojia yaliyojitokeza katika kazi zao.

#### **3.3 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika mkoani Kagera katika wilaya ya Manispaa Bukoba, katika wilaya hii ni kata nne tu kati ya kata kumi na nne zilizohusika katika utafiti huu. Kata zilizohusika pamoja na shule zake ni Kata ya Kitendaguro (shule ya msingi Kitendaguro na Bugambakamoi), Kata Buhembe (shule ya msingi Kashenge). Kata Ijuganyondo (shule ya Msingi Ibura) na Kata Kahororo (shule ya msingi Kahororo).

Kata hizi zilichaguliwa na mtafiti ili kuwa eneo lake la utafiti kwa sababu kata hizo zipo pembezoni mwa mji na wakazi wake hutumia sana lugha ya Kihaya katika mawasiliano yao kwa muda mwingi, hivyo wengi hujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu wawapo shuleni.

### **3.4 Sampuli na Usampulishaji**

Katika kipengele hiki idadi ya watafitiwa au wasailiwa imewekwa bayana, vilevile mbinu zilizotumika kuwapata wasailiwa au watafitiwa nazo zimewekwa wazi na mtafiti.

#### **3.4.1 Sampuli**

Katika utafiti huu kundi lengwa lilikuwa ni wazungumzaji na wataalamu wa lugha ya Kiswahili na Kihaya. William (2011) anafafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika utafiti (vinavyotafitiwa) yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa ujumla, kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Kothari (2004:55), anaelezea kuwa, uteuzi wa walengwa ni mbinu au utaratibu ambao mtafiti atatumia katika kuchagua orodha ya vitu au watu kwa ajili ya sampuli. Walengwa wa utafiti huu waligawanywa katika makundi matatu, kundi la kwanza ni wanafunzi 70 wa shule za msingi tano zilizopo Manispaa ya Bukoba.

Mtafiti alikutana na walengwa 14 kwa kila shule ambao wanajua kuongea lugha ya Kihaya na kwa sasa wanajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Kundi hili liliateuliwa kwa sababu wao hutumia lugha ya Kihaya wawapo nyumbani na vile vile hujifunza Kiswahili sanifu wawapo shuleni. Hivyo ni rahisi kwa mtafiti kupata data

yake ya utafiti. Watafitiwa na kundi la pili walikuwa ni walimu 15 wanaofundisha somo la Kiswahili, Hisabati, Uraia na Maadili na Jiografia katika shule hizo tano. Hivyo mtafiti alikutana na walimu 3 kwa kila shule. Kundi la tatu ni wazazi 10 ambao wanajua lugha ya Kihaya na Kiswahili sanifu. Kundi hili lilitolewa kwa sababu ndio huwa na wanafunzi baada ya muda wa masomo na vile vile ndio watumiaji wa lugha ya Kihaya kwa muda mwingi. Vile vile kundi hili la tatu lina umilisi wa lugha zote mbili Kiswahili na Kihaya, hivyo ilikuwa rahisi kwa mtafiti kuweza kutambua sababu za wanafunzi wanaozungumza Kihaya kufanya makosa ya kifonolojia katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu.

### **3.4.2 Mbinu za Usampulishaji**

Mtafiti aliteua sampuli ya utafiti kulingana na sifa ya kuwa wana uwezo wa kutoa data sahihi zilizotakiwa kulingana na lengo la utafiti huu yaani waliokuwa na uwezo wa kutoa habari faafu zilizojibu kikamilifu maswali ya utafiti. Babbie (1999) anasema kwamba, sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutiwa nayo katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa.

Katika utafiti huu watafitiwa 95 waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa (wa makusudio), usampulishaji nasibu na usampulishaji kutajana. Miongoni mwao, watafitiwa 70 walikuwa wanafunzi wa shule za msingi ambao wanaonea lugha ya Kihaya ila kwa sasa wanajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili ambao waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa (wa kimakusudi) na usampulishaji nasibu. Katika usampulishaji nasibu mtafiti aliandaa vikaratasi vidogo vidogo

vilivyoandikwa òndiyoò na òhapanaò na kuvichanganya changanya na kisha kuvitupa chini na kuwataka wanafunzi waokote vikaratasi hivyo.

Waliookota vikaratasi vilivyoandikwa neno òndiyoò hao ndiyo waliohusika kama watafitiwa wa utafiti huu. Watafitiwa 15 walikuwa walimu wa shule 5 za msingi ambao waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu na usampulishaji kutajana. Watafitiwa 10 walikuwa wazazi wanaozungumza lugha Kihaya na Kiswahili wenye umri kati ya miaka 45 hadi 80. Hawa waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa na usampulishaji kutajana.

**Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Watafitiwa**

<b>Na.</b>	<b>Kundi la watafitiwa</b>	<b>Idadi ya watafitiwa</b>
1.	Wanafunzi wanaozungumza Kihaya wanaojifunza Kiswahili	70
2.	Walimu wanaowafundisha wanafunzi wa shule za msingi wanaozungumza Kihaya ila wanajifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili	15
3.	Wazazi wanaozungumza lugha ya Kihaya na Kiswahili	10
<b>Jumla</b>		<b>95</b>

Mtafiti alichagua watafitiwa kwa idadi kama walivyo katika makundi kutokana na sababu zifuatazo:

Mtafiti alichagua watafitiwa 70 ambao ni wanafunzi kwa sababu watafitiwa hawa ndiyo watendaji wakubwa wa makosa ya kifonolojia. Vile vile kundi hili limekuwa na watafitiwa wengi kuliko makundi mengine kwa sababu makosa yaliyochunguzwa ni yale yaliyojirudia zaidi ya mara moja kwa mtafitiwa mmoja, hivyo mtafiti alihitaji watafitiwa wengi katika kundi hili ili iwe rahisi kupata data sahihi ya utafiti.

Pia mtafiti alichagua watafitiwa 15 ambao ni walimu kwa sababu ya muda wa upatikanaji wao. Wengi wao walionekana kubanwa na kazi zao za ufundishaji. Hivyo kama mtafiti angelichagua watafitiwa wengi kwa upande wa walimu angelitumia muda mwingi sana kukusanya data yake ya utafiti ikiwa ni pamoja kwenda eneo moja mara kwa mara kwa ajili ya kugawa hojaji na kufanya mahojiano nao.

Vile vile mtafiti alichagua watafitiwa 10 ambao ni wazazi wenye umilisi wa Kihaya na Kiswahili. Mtafiti alichagua idadi hii kwa sababu ya ugumu wa upatikanaji wa watafitiwa. Watafitiwa ambao ni wazazi wenye umilisi wa Kihaya na Kiswahili ni wachache sana nao walipatikana kwa mbinu ya kutajana. Hivyo, kama mtafiti angelichagua kundi kubwa katika kundi hili angelitumia muda mwingi sana kukusanya data yake ya utafiti.

### **3.5 Njia za Ukusanyaji wa Data**

Utafiti huu ulitumia njia mbalimbali katika kukusanya data ya utafiti ili kuweza kupata data sahihi kulingana na malengo ya utafiti husika na walengwa wa utafiti. Njia zilizotumika kukusanya data ni pamoja na hojaji, mahojiano na usomaji makini.

#### **3.5.1 Hojaji au Dodoso**

Kothari (2004), hojaji ni njia ya kukusanya data ambayo mtafiti huandika maswali na baadaye huwapa watoa taarifa ili wayajibu na kumrudishia. Kwa mujibu wa Williman (2011) anaeleza kuwa, kuna maswali ya hojaji ya aina mbili. Aina ya kwanza ni maswali funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jawabu. Aina hii ni rahisi kujibu na kuchanganua. Pia, inasaidia kupata majibu mahususi na huepusha

upendeleo. Aina ya pili ya maswali ya hojaji yasiyo funge, ambayo hutoa fursa au uhuru kwa watafitiwa kueleza wanachokijua.

Aidha, husaidia kupata taarifa nyingi zaidi. Aina ya hojaji iliyotumika katika utafiti huu ilijumuisha aina zote mbili za maswali yaliyokuwemo katika hojaji, maswali funge na maswali yasiyofunge. Mtafiti aliamua kuchanganya aina zote za maswali ili kuepuka kasoro zinazoweza kutokea katika aina hizi mbili, ikizingatia kuwa kila moja ina kasoro zake. Hivyo, aina hizo zilitumika kwa pamoja ili kukamilishana. Mtafiti aliwapa watafitiwa wake ambao ni wanafunzi, walimu na wazazi wanaozungumza Kihaya na Kiswahili hojaji wajaze papo kwa papo na kisha warejeshe kwa ajili ya uchambuzi wa data. Njia ya hojaji ilichaguliwa kwa sababu inafaa kukusanya data katika kundi kubwa la watu na kwa muda mfupi sana hasa hojaji za papo kwa papo. Aidha, ni njia rahisi na ya haraka katika kukusanya na kuchanganua data. Pia, ikisimamiwa vizuri data nyingi zinaweza kupatikana kwa muda mfupi. Data zilizopatikana kwa njia hii zilisaidia kujibu maswali matatu ya utafiti ambayo yaliuliza:

- (i) Ni makosa gani ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu?
- (ii) Je, nini kinasababisha wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa hayo katika kujifunza Kiswahili sanifu?
- (iii) Mbinu gani zitumike ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu?

Swali la pili na la tatu katika njia ya hojaji yalijibiwa kwa ufupi sana, hivyo maelezo yake yalipatikana kwa kutumia njia ya mahojiano ili kukamilisha data ya utafiti.

### 3.5.2 Mahojiano

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana (au simu, barua pepe) kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililo ainishwa. Williman (2011) ameyagawa mahojiano katika aina mbili ambazo ni, mahojiano ya ana kwa ana na mahojiano ya simu (mtandao) Ingawa njia hii inaweza kufanywa kwa njia zote hizo, mtafiti alitumia njia ya kuwahoji watafitiwa ana kwa ana. Kwa mujibu wa Kothari (1990), mahojiano ya ana kwa ana ni mbinu ambayo mtafiti huwauliza watafitiwa maswali na wakati mwingine watafitiwa nao huuliza maswali na mtafitiwa huyajibu. Mbinu hii ilitumika kwa watafitiwa ambao ni walimu na wazazi wanaozungumza Kihaya na Kiswahili. Njia hii ilitumiwa kwa sababu ya kupata uthabiti wa majibu ya watafitiwa. Pili, ni rahisi kwa mtafiti kudhibiti sampuli kwa usahihi zaidi.

Hii iliwezekana kwa sababu mtafiti alikutana na wahojiwa ana kwa ana na kuwauliza maswali. Maswali ambayo yalionekana kukosa majibu, yalitafutiwa ufumbuzi papo kwa papo. Tatu ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi na kwa kina zaidi, kwa sababu watafitiwa waliweza kuuliza maswali na mtafiti alikuwa na uhuru wa kuuliza maswali zaidi ambayo ni vigumu kufanyika kwa kutumia mbinu nyingine kama vile ushuhudiaji, ushiriki au hojaji. Mbinu hii ilisaidia katika uchanganuzi wa data yetu na hata katika utoaji wa mahitimisho.

Data zilizopatikana kwa njia hii zilisaidia kujibu maswali mawili ya utafiti ambayo;

- (i) Je, nini kinasababisha wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa ya kifonolojia katika kujifunza Kiswahili sanifu?

- (ii) Mbinu gani zitumike ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu?

### **3.5.3 Usomaji Makini**

Katika njia hii, mtafiti alipitia kwa umakini kazi andishi za wanafunzi ndani ya madaftari yao. Kazi hizi ni zile ambazo walimu huwapatia wanafunzi wazifanye na kisha kusahihishwa na walimu. Mtafiti alipitia kazi nne kwa kila mwanafunzi. Mtafiti alinukuu makosa katika shajara lake na makosa mengine kuyapiga picha alipoyabaini. Kwa kutumia njia ya usomaji makini kosa lilihesabika kama kosa iwapo kosa hilo la kifonolojia lilijirudia zaidi ya mara moja. Njia hii ya utafiti ilisaidia kupatikana kwa data sahihi ya utafiti.

Njia ya usomaji makini ilisaidia kujibu swali lililouliza; ni makosa gani ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu? Swali hili lilikamilisha lengo la utafiti ambalo lilikuwa; kubainisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu.

### **3.6 Vifaa vya Kukusanyia Data**

Mtafiti aliandaa vifaa vya utafiti kulingana na mada na malengo ya utafiti. Vifaa hivi vilimwezesha mtafiti kukusanya data husika na kupata taarifa sahihi za utafiti wake.

#### **(i) Shajara**

Kifaa hiki kilimsaidia mtafiti katika kunukuu na kuhifadhi baadhi ya data za msingi kama vile taarifa za wahojiwa, data za msingi na data fuatizi katika utafiti huu.



**(ii) Kinasa Sauti**

Kifaa hiki kilitumika katika kunasa na kurekodi sauti wakati wowote katika miktadha mbalimbali hivyo mtafiti alikitumia kurekodi mahojiano baina yake na watafitiwa. Taarifa zilizorekodiwa zilitumika katika uchambuzi wa data katika utafiti huu.

**(iii) Kompyuta**

Ilitumika katika kutafutia matini kutoka katika tovuti na pia kuhifadhi taarifa mbalimbali. Data zilihifadhiwa, zilichambuliwa na kutolewa hitimisho kisha kutumika katika kuandaa ripoti ya utafiti. Pia kompyuta ilitumika kama sehemu ya maktaba tembezi.

**(iii) Kinyonyi**

Hiki kilitumika kuhifadhia data mbalimbali.

**3.7 Uchambuzi wa Data**

Kothari (1990), anaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Data zilikusanywa kutoka katika vyanzo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Mtafiti kwa kutumia mkabala wa kinaelezo alichambua data hizo. Uchambuzi huu wa data ulifuata hatua zifuatazo:

- (i) Kuorodhesha maneno au sentensi zenye makosa
- (ii) Kuainisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu
- (iii) Katika hatua ya tatu, mtafiti alieleza sababu kosa

- (iv) Hatimaye, mtafiti alitathmini kiwango cha kosa na kuweza kupendekeza mbinu za kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Data zilizochambuliwa katika utafiti huu, zimekusanywa kwa njia kuu tatu ambazo ni hojaji, usomaji makini na mahojiano. Kupitia hojaji, mtafiti alipata data ya makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu, sababu za makosa na mbinu za kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Data zilizokusanywa kwa njia ya hojaji zilichambuliwa kwa njia ya kimaelezo.

Kupitia njia ya usomaji makini, mtafiti alipata data ya makosa yanayofanywa na wanafunzi ambapo data hizi zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Njia nyingine ni njia ya mahojiano, mtafiti kupitia njia hii alipata data ya sababu za makosa na mbinu za kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu ambazo nazo zilichambuliwa kwa njia ya maelezo.

### **3.8 Muhtasari**

Katika sura hii ya tatu, mtafiti ameweza kueleza aina ya utafiti alioufanya, eneo ambapo utafiti wake ulifanyika, sampuli na usampulishaji yaani idadi ya watu waliohusika katika kutoa data ya utafiti na mbinu zilizotumika kuwapata watafitiwa, njia za kukusanyia data ambapo hojaji, mahojiano, na usomaji makini zilitumika, vile vile vifaa vya kukusanyia data viliainishwa pamoja na mkabala ulikaotumika katika uchambuzi wa data uliwekwa bayana.

## SURA YA NNE

### UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Sura hii ni ya uwasilishaji wa data ya makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Data ya utafiti huu imekusanya nyanjani kwa kutumia njia kuu tatu ambazo ni hojaji, mahojiano na usomaji makini. Data hii ilikusanywa kutokana na sampuli ya wanafunzi wa darasa la nne na la tatu wanaozungumza Kihaya kwa sasa wanajifunza Kiswahili sanifu katika shule ya msingi Ibura, Kitendaguro, Bugambakamoi, Kahororo na Kashenge katika Manispaa ya Bukoba. Vile vile data hii imekusanywa kwa walimu wanaowafundisha wanafunzi hao pamoja na wazazi wenye umilisi wa lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili.

Uwasilishaji wa matokeo umefanyika kwa kutumia misingi ya nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na Corder (1967) ili kubainisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Uwasilishaji wa matokeo haya unalenga kujibu maswali ya utafiti ili kukamilisha malengo ya utafiti. Aidha, sura hii inawasilisha matokeo na kuyajadili kwa mujibu wa data iliyochambuliwa na hoja mbalimbali za wataalamu kama zilivyo kwenye mapitio ya kazi tangulizi za tasnifu hii.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne, ambazo ni:

- (i) Utambuzi wa makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

- (ii) Uchambuzi wa makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.
- (iii) Uwasilishaji na ufafanuzi wa sababu za wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa ya kifonolojia katika kujifunza Kiswahili sanifu.
- (iv) Uwasilishaji wa mapendekezo ya mbinu za kutumia ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili.

#### **4.2 Utambuzi wa Makosa**


Katika sehemu hii tumechambua data iliyokusanywa kwa usomaji makini. Mtafiti alisoma kwa makini kazi mbalimbali za wanafunzi zilizomo katika madaftari yao na kubaini kuwa yapo makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Katika utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa makosa ya kisauti yalijitokeza zaidi katika sauti konsonanti ambapo wanafunzi waliochunguzwa ambao huzungumza Kihaya kama lugha yao ya kwanza waligeuza baadhi ya sauti konsonanti za Kiswahili sanifu kwa kuzitumia kama wanavyozitumia konsonanti hizo katika lugha ya Kihaya.

#### **Kwa mfano:**

Sauti Konsonanti /g/ ilitumika badala ya /gh/,


neni òghaliö liliandikwa ògaliö



**Kielelezo Na. 4.1: Kuonesha Matumizi ya Sauti /g/ Badala ya Sauti /gh/**

Sauti konsonanti /ng/ ilitumika badala ya /ngø/


neni òngøombeö liliandikwa òngombeö



**Kielelezo Na. 4.2: Kuonesha Matumizi ya Sauti /ng/ Badala ya Sauti /ng'/ na Uchopekaji wa Sauti /u/**


Sauti konsonanti /z/ ilitumika badala ya /dh/

Neno òdhaifuö liliandikwa òzaifuö



**Kielelezo Na. 4.3: Kuonesha Matumizi ya Sauti /z/ Badala ya Sauti /dh/**

Sauti konsonanti /s/ ilitumika badala ya /th/. Neno òthelethiniö liliandikwa òselasiniö




**Kielelezo Na. 4.4: Kuonesha Matumizi ya Sauti /s/ Badala ya Sauti /th/**

Pia, mtafiti alitambua kuwa baadhi ya wanafunzi waliochunguzwa kupitia kazi zao walidondosha baadhi ya sauti irabu na konsonanti kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu.


**Kwa mfano:**

Katika neno òmahusianoö sauti /h/ ilidondoshwa na neno hilo kuandikwa òmausianoö



**Kielelezo Na. 4.5: Kuonesha Udondoshaji wa Sauti /h/**

Katika neno òmudaö sauti irabu /u/ ilidondoshwa na neno hilo kuandikwa òmdaö




**Kielelezo Na. 4.6: Kuonesha Udondoshaji wa Sauti /u/**

Vile vile, mtafiti alitambua kuwa kuna uchopekaji wa baadhi sauti konsonanti na sauti irabu katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu.

**Kwa mfano;**


Katika neno òmsaadaö kulichopekwa sauti /h/ na kuandikwa òmsahadaö

Katika neno òmkulimaö kulichopekwa sauti /u/ na kuandikwa òmukulimaö



#### Kielelezo Na. 4.7: Kuonesha Uchopekaji wa Sauti /h/ na /u/

Aidha, kupitia utafiti huu, mtafiti alitambua kuwepo na wanafunzi wanaochanganya baadhi ya sauti. Watafitiwa wengi kwa upande wa wanafunzi hasa waliofanyiwa uchunguzi walibainika kuchanganya sauti /r/ na /l/, sauti /th/ na /dh/, sauti /a/ na /h/



#### Kielelezo Na. 4.8: Kuonesha Kuchanganya Sauti /l/ na /r/

Makosa haya ya kisauti huibua utata wa kimaana ambapo wakati mwingine maana huweza kupotea kabisa au kuvurugwa.



### 4.3 Uchambuzi wa Makosa

Mtafiti alichambua makosa ambayo yalionekana kujirudia rudia mara kwa mara kwa kila mwanafunzi aliyechunguzwa. Mtafiti ameonyesha makosa na kuonyesha ni kipi alichotaka kusema kutokana na taratibu za lugha legwa. Makosa ya kifonolojia yaliyobainishwa na kuchambuliwa ni pamoja na matumizi ya sauti mbadala, kuchanganya sauti, kudondosha sauti na uchopekaji wa sauti. Makosa hayo yamechambuliwa kama ifuatavyo:

#### 4.3.1 Matumizi ya Sauti Mbadala

Mtafiti amebaini kuwa baadhi ya sauti za lugha ya Kiswahili ambazo hazipo katika mfumo wa sauti za lugha ya Kihaya huwashinda wanafunzi kuzitamka na hata kuziandika wakati wanapoandika Kiswahili sanifu. Sauti hizo ni pamoja na sauti /gh/, /th/, /dh/, /v/ na /ng $\emptyset$ .

##### 4.3.1.1 Matumizi ya Sauti /g/ Badala ya /gh/

Sauti /gh/ haipatikani katika mfumo wa sauti za lugha ya Kihaya badala yake kuna sauti /g/. Jambo linalozua utata zaidi ni uwakilishaji wa sauti /g/ kama sauti /gh/ kimatamshi na kimaandishi katika lugha ya Kiswahili sanifu.

#### Jedwali Na. 4.1: Kuonesha Matumizi ya Sauti /g/

Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilisho wa Kifonetiki	Kiswahili sanifu	Uwakilisho wa Kifonetiki
gorofa	/gorofa/	ghorofa	/ orofa/
Gali	/gali/	ghali	/ ali/
Gala	/gala/	ghala	/ ala/
shuguli	/shuguli/	shughuli	/ u uli/

Kipasuo ghuna /g/ kinapatikana katika mfumo wa sauti wa lugha ya Kihaya na Kiswahili ila kikwamizo cha kaakaa laini /gh/ hakipo katika mfumo wa sauti za lugha ya Kihaya ila sauti hiyo ipo katika mfumo wa sauti za lugha ya Kiswahili sanifu. Mtafiti alibaini kuwa sauti hizi hutamkiwa kwenye kaakaa laini, hivyo wanafunzi waliochunguzwa walionekana kutaka kurahisisha mfumo wa sauti wa lugha lengwa. Hali hii inachangia kuwepo kwa makosa ya Kifonolojia kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

#### 4.3.1.2 Matumizi ya Sauti /s/ Badala /th/

Mtafiti alibaini kuwa katika mfumo wa sauti wa lugha ya Kihaya hakuna sauti /th/ badala yake kuna sauti /s/ ambayo ina ufanano wa karibu sana kimatamshi na sauti /th/. Hivyo wanafunzi wanaozungumza Kihaya kama L1 kwao na kwa sasa wanajifunza Kiswahili kama L2 yao hutumia sauti /s/ badala ya /th/ wanapozungumza au kuandika kiswahili sanifu.

**Jedwali Na. 4.2: Kuonesha Matumizi ya Sauti /s/**

Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilisho wa Kifonetiki	Kiswahili sanifu	Uwakilisho wa Kifonetiki
selasini	/selasini/	thelathini	/ ela ini/
samani	/samani/	thamani	/ amani/
Asari	/asari/	athari	/a ari/
semanini	/semanini/	themanini	/ emanini/
tasimini	/tasimini/	tathmini	/ta mini/

Sauti /s/ na /th/ zina sifa zinazofana kifonolojia ambapo sauti hizi zote ni vikwamizo si ghuna. Hivyo katika mfumo wake wa ufundishaji wanafunzi huweza kuzifananisha kimatamshi, hivyo kusababisha makosa ya kifonolojia.

#### 4.3.1.3 Matumizi ya Sauti /z/ Badala ya /dh/

Vile vile lugha ya Kihaya haina sauti /dh/. Wanafunzi waliochunguzwa walionekana kutumia sauti /z/ badala ya /dh/

#### Jedwali Na. 4.3: Kuonesha Matumizi ya Sauti /z/

Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilisho kifonetiki	Kiswahili sanifu	Uwakilisho kifonetiki
Zaifu	/zaifu/	dhaifu	/ðaifu/
zambi	/zambi/	dhambi	/ðambi/
zamini	/zamini/	dhamini	/ðamini/
zibiti	/zibiti/	dhibiti	/ðibiti/

Katika hali ya ufundishaji wanafunzi walionekana kushindwa kutofautisha sauti /z/ na /dh/. Hii ni kutokana na sauti hizi kuwa na ufanano wa kifonetiki ambapo sauti hizi zote ni vikwamizo ghuna.

#### 4.3.1.4 Matumizi ya Sauti /ng/ Badala ya /ngʻ/

Katika lugha ya Kihaya sauti /ngʻ/ haipo badala yake wanafunzi waliochunguzwa hutumia sauti ya silabi /ng/ kama mbadala wake wakati wa kuzungumza na kuandika kiswahili sanifu.

#### Jedwali Na. 4.4: Kuonesha Matumizi ya Sauti /ng/

Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilisho wa kifonetiki	Kiswahili sanifu	Uwakilisho wa kifonetiki
ngombe	/ngombe/	Ngømbe	/ ombe/
Ngoa	/ngoā/	Ngøā	/ oa/
ngangania	/ngangania/	Ngøangøania	/ a ania/
Ngaa	/ngaa/	Ngøaa	/ aa/

Hali hii inatokana na wanafunzi kutaka kurahisisha muundo wa sauti na silabi za lugha lengwa.

### 4.3.2 Kuchanganya Sauti

Utafiti huu umebaini kuwa watafitiwa (wanafunzi) hawana umilisi wa kutosha katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wanashindwa kutofautisha baadhi ya sauti za Kiswahili sanifu hasa katika maandishi. Sauti zinazochanganywa zipo kama ifuatavyo:

#### 4.3.2.1 Kuchanganya Sauti /a/ na /h/

Mtafiti alibaini kuwa wanafunzi wanachanganya sauti irabu /a/ na sauti konsananti /h/ wakati sauti irabu /a/ na sauti konsonanti /h/ zote zipo katika mfumo wa sauti za lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili. Kwa wanafunzi waliochunguzwa ilionekana hawajui ni wakati gani sauti irabu /a/ inatumika na ni wakati gani sauti /h/ inatumika katika maandishi ya Kiswahili sanifu.

#### Jedwali Na. 4.5: Kuonesha Matumizi ya Sauti /a/

Mifani ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilisho kifonetiki	Kiswahili sanifu	Uwakilisho kifonetiki
Arusi	/arusi/	harusi	/harusi/
apana	/apana/	hapana	/hapana
mtiani	/mtiani/	mtihani	/mtihani/
watahalamu	/watahalamu/	wataalamu	/wataalamu/
maharifa	/maharifa/	maarifa	/maarifa/

Hali hii ya kuchanganya sauti irabu /a/ na sauti konsonanti /h/ kunatokana na matamshi ya walimu wenyewe pamoja na sauti hizi kuwa na ufanano wa karibu sana

kimatamshi ambapo sauti hizi zote hutamkwa wakati ulimi ukiwa chini na mdomo ukiwa katika hali mtandazo.

#### 4.3.2.2 Kuchanganya Sauti /r/ na Sauti /l/

Katika utafiti huu, mtafiti amebaini kuwa baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kihaya huchanganya sauti /r/ na sauti /l/ wakati wanapoandika Kiswahili sanifu. Sauti hizi mbili /r/ na /l/ zipo katika lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili kama sauti hizo zilivyoainishwa katika sura ya pili ya tasnifu ya utafiti huu.

**Jedwali Na. 4.6: Kuonesha Matumizi Ya Sauti /r/**

Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilisho kifonetiki	Kiswahili sanifu	Uwakilisho kifonetiki
Mrevi	/mrevi/	mlevi	/mlevi/
Karamu	/karamu/	kalamu	/mlevi/
Mshare	/m are/	mshale	/m ale/
Kurowa	/kurowa/	kulowa	/kulowa/
Dalaja	/dalaja/	daraja	/daraja/
Ishilini	/i ilini/	ishirini	/i irini/
Ledio	/ledio/	redio	/redio/
Kalibu	/kalibu/	karibu	/karibu/
Fauru	/fauru/	faulu	/faulu/

Makosa haya hutokana na ufundishaji usiofaa. Vilevile hutokea kutokana na ufanano wa karibu mno wa sauti hizi mbili kimatamshi ambapo sauti zote mbili hutamkwa kwa ncha ya ulimi kugusa ufizi. Hivyo wanafunzi hushindwa kujua ni wakati gani sauti /r/ hutumika na ni wakati gani sauti /l/ hutumika.

#### 4.3.2.3 Kuchanganya Sauti /th/ na Sauti /dh/

Mtafiti amebaini kuwa pamoja na lugha ya Kihaya kutokuwa na sauti za vikwamizo vya meno /th/ na /dh/ wapo wazungumzaji wa Kihaya wanaoshindwa kabisa kuzitofautisha sauti hizi wanapoandika Kiswahili sanifu.

**Jedwali Na. 4.7: Kuonesha Matumizi ya Sauti /th/**

Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilisho kifonetiki	Kiswahili sanifu	Uwakilisho kifonetiki
walithoofika	/wali oofika/	walidhoofika	/waliðoofika/
Thambi	/ ambi/	dhambi	/ðambi/
Thibiti	/ ibiti/	dhibiti	/ðibiti/
Adhari	/aðari/	athari	/a ari/
Dhamani	/ðamani/	thamani	/ amani/
Miradhi	/miraði/	mirathi	/mira i/

Hapa kuna makosa yanayotokana na ufundishaji usiofaa kwamba wanafunzi wamerithishwa makosa jambo ambalo linakuwa gumu kwa kulifahamu. Hali hii husababisha wanafunzi kuchanganyikiwa bila kujua ni sauti ipi kati ya hizi mbili inafaa kutumika. Hata hivyo, sauti /th/ na sauti /dh/ zina ufanano wa karibu sana ambapo sauti hizi hutamkika kwenye meno (mahali pa matamshi) na vile vile katika jinsi ya kutamka sauti zote ni vikwamizo isipokuwa tu kwamba sauti /dh/ ni ghuna na sauti /th/ si ghuna. Mwanafunzi anapotumia sauti mojawapo badala ya nyenzake, hutokana na ufanano wa sifa zake za kifonetiki.

#### 4.3.2.4 Kuchanganya Sauti /a/ na /w/

Mtafiti amebaini wanafunzi wanaozungumza Kihaya huchanganya sauti irabu /a/ na sauti konsonanti /w/ wakati wa kuandika Kiswahili sanifu.

**Jedwali Na. 4.8: Kuonesha Matumizi ya Sauti /a/**

<b>Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi</b>	<b>Uwakilisho kifonetiki</b>	<b>Kiswahili sanifu</b>	<b>Uwakilisho kifonetiki</b>
Uwa	/uwa/	ua	/ua/
Kua	/kua/	kuwa	/kuwa/
Hua	/hua/	huwa	/huwa/
Uanja	/uanja/	uwanja	/uwanja/
Kukuwa	/kukuwa/	kukua	/kukuwa/

Makosa haya yanatokana na ufanano wa kimatamshi wa sauti Irabu /a/ na sauti konsonanti /w/. sauti irabu /a/ hutamkwa bila kuwepo na kizuizi chochote cha mkondo hewa kutoka mapafuni na konsonanti /w/ hutamkwa huku kukiwa na mzuio mdogo wa hewa. Sauti hizi pia hutamkwa wakati mdomo ukiwa katika hali ya wazi na hivyo kuwa na ufanano wa karibu wa kifonetiki.

**4.3.3 Uchopekaji wa Sauti**

Uchopekaji ni hali ya mzungumzaji kuongeza sauti fulani katika neno na kufanya neno hilo kupoteza sifa yake kimatamshi. Uchopekaji uliobainishwa kutoka kwa watafitiwa upo kama ifuatavyo;

**4.3.3.1 Uchopekaji wa Sauti /h/**

Wanafunzi waliochunguzwa walionekana kuchopeka kiholela sauti konsonanti /h/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Konsonanti /h/ imo katika mfumo wa sauti ya lugha ya Kihaya pamoja na lugha ya Kiswahili.

**Jedwali Na. 4.9: Kuonesha Matumizi ya Sauti /h/**

<b>Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi</b>	<b>Uwakilisho kifonetiki</b>	<b>Kiswahili sanifu</b>	<b>Uwakilisho kifonetiki</b>
Wanahishi	/wanahi i/	wanaishi	/wanai i/
Mshada	/msahada/	msaada	/msaada/
Hibariki	/hibariki/	ibariki	/ibariki/
Habiria	/habiria/	abiria	/abiria/
Sitahisahau	/sitahisahau/	sitaisahau	/sitaisahau/
Hilikuwa	/hilikuwa/	ilikuwa	/ilikuwa/
Hawali	/hawali/	awali	/awali/
Hile	/hile/	ile	/ile/
Hurafiki	/hurafiki/	urafiki	/urafiki/
Rahia	/rahia/	raia	/raia/

Kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu inaonekana kuwa wanafunzi walichopeka sauti /h/ mwanzoni mwa neno kama katika õhilikuwaõ na katikati mwa neno kama ilivyo katika neno õsitahisahauõ. Uchopekaji wa sauti /h/ hutokea kabla ya Irabu. Kwa hiyo wanafunzi walichanganyikiwa ni wakati upi sauti /h/ inafaa kutumiwa na ni lini haifai. Hali hii inatokana na juhudi za wanafunzi kurahisisha miundo ya lugha lengwa (Kiswahili).

**4.3.3.2 Uchopekaji wa Sauti /u/ na /i/ Katika Silabi Funge Silabi za Konsonati****Pekee**

Matinde (2012) anasema silabi fungu ni silabi ambazo huishia kwa konsonanti. Hivyo katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu kuna maneno yenye silabi fungu ambapo mtafiti amegundua kuwa baadhi ya wanafunzi huchopeka irabu /i/ au /u/ katika silabi fungu za Kiswahili sanifu. Hii husababisha utamkaji tofauti wa neno husika.



**Jedwali Na. 4.10: Kuonesha Uchopekaji wa Sauti /u/ na /i/**

<b>Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi</b>	<b>Uwakilisho kifonetiki</b>	<b>Kiswahili sanifu</b>	<b>Uwakilisho kifonetiki</b>
Hamusini	/hamusini/	hamsini	/hamsini/
Mukulima	/mukulima/	mkulima	/mkulima/
Dakitari	/dakitari/	daktari	/daktari/
Mutu	/mutu/	mtu	/mtu/
Kabula	/kabula/	kabla	/kabla/
Labuda	/labuda/	labda	/labda/
Asikari	/asikari/	askari	/askari/
Dafutari	/dafutari/	daftari	/daftari/
Afirika	/afirika/	afrika	/afrika/
Mujini	/mujini/	mjini	/mjini/
Elufu	/elufu/	elfu	/elfu/

Maneno mengi yenye silabi funge ni yale maneno ya mkopo yaliyoingizwa katika lugha ya Kiswahili kutoka katika lugha nyingine ulimwenguni. Pia kuna silabi za konsonanti pekee za maneno ya Kiswahili ambapo sauti za nazali huweza kusimama pekee yake kama silabi. Hii ni tofauti na sauti za lugha ya Kihaya ambayo haina silabi funge na silabi za konsonanti pekee. Kwahiyo kosa hili bila shaka linatokana na athari ya L1 iliyo na muundo tofauti wa silabi na L2.

#### **4.3.4 Udondoshaji wa Sauti**

Udondoshaji ni hali ya mzungumzaji au mwandishi kuacha baadhi ya vitamkwa au sauti na kufanya neno husika litamkike kimakosa. Udondoshaji uliofanya na watafitiwa ulikuwa kama ifuatavyo:

#### 4.3.4.1 Udondoshaji wa Sauti /h/

Wanafunzi waliochunguzwa walionekana kudondosha sauti /h/ wakati wa kuandika Kiswahili sanifu, hivyo kupata miundo isiyo sahihi ya maneno ya Kiswahili sanifu.

**Jedwali Na. 4.11: Kuonesha Matumizi ya Sauti /h/**

Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilisho kifonetiki	Kiswahili sanifu	Uwakilisho kifonetiki
Ana	/ana/	hana	/hana/
Ataki	/ataki/	hataki	/hataki/
Eshima	/eshima/	heshima	/he ima/
Awiki	/awiki/	hawiki	/hawiki/
Akosi	/akosi/	hakosi	/hakosi/
Asubui	/asubui/	asubuhi	/asubuhi/
Amsini	/amsini/	hamsini	/hamsini/
Roo	/roo/	roho	/roho/
Uzuni	/uzuni/	huzuni	/huzuni/

Sauti /h/ ipo katika mfumo wa lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili. Hali hii inatokana na kile ambacho Corder (1967) anakiita ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa. Udondoshaji wa sauti /h/ unapofanywa hususani pale ambapo mwanafunzi alipolenga kukanusha maana kusudiwa upotea. Kwa mfano mwanafunzi alilenga kusema òmtoto huyu hana usingiziö akaishia kusema òmtoto huyu ana usingiziö. Mtafiti amegundua kuwa udondoshaji wa sauti /h/ miongoni mwa wanafunzi wanaozungumza Kihaya na kwa sasa wanajifunza Kiswahili sanifu kunatokana na hali ya kutokuwa na uelewa wa kina juu ya matumizi ya sauti hii, hali inayopelekea wanafunzi kuchanganyikiwa na kukosa kujua watumie sauti hiyo wapi.

#### 4.3.4.2. Udondoshaji wa Sauti /u/

Vile vile mtafiti anabainisha kuwa kuna udondoshaji wa sauti irabu /u/ wa unaofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Udondoshaji huu huibua muundo tofauti wa lugha lengwa.

**Jedwali Na. 4.12: Kuonesha Udondoshaji wa Sauti /u/**

Mifano ya makosa kutoka kwa wanafunzi	Uwakilishi kifonetiki	Kiswahili	Uwakilishi kifonetiki
Mda	/mda/	Muda	/muda/
Kalam	/kalam/	Kalamu	/kalamu/
Msa	/msa/	Musa	/musa/
Mziki	/mziki/	Muziki	/muziki/

Makosa haya ya udondoshaji wa sauti /u/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Inaonekana hutoana na mkakati wa kujifunza L2 wanafunzi wanapajaribu kusahihisha miundo ya L2 ambampo tayari wamejifunza silabi funge na silabi za kunsonanti pekee. Hivyo udondoshaji wao ufanyika katika mazingira yasiyo rasmi.

#### 4.4 Sababu za Kufanya Makosa ya Kifonolojia

Kipengele hiki kimefafanua sababu zinazopelekea kufanya makosa ya kifonolojia kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Sababu hizi zimekusanywa nyanjani kwa kutumia njia ya hojaji na njia ya mahojiano. Njia hizi mbili zilitumika kwa sababu katika njia ya hojaji watafitiwa walitaja tu sababu bila ufafanuzi wa kutosha, hivyo kupitia njia ya mahojiano watafitiwa waliweza kutoa maelezo ya sababu hizo na mtafiti kupata data ya kutosha. Watafitiwa waliohusika katika kutoa sababu zinazopelekea kufanya makosa ya kifonolojia kwa wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu ni pamoja walimu na wazazi wenye umilisi wa Kihaya

na Kiswahili sanifu kama walivyotajwa katika sura ya tatu kipengele cha 3.3. Sababu hizo kama ifuatavyo:

- (i) Utofauti wa mfumo wa sauti konsonanti kati ya Kihaya na kiswahili sanifu. Katika mahojiano yaliyofanywa kati ya mtafiti na walimu, walimu tisa kati ya walimu kumi na tano waliohojiwa walisema kuwa ðbaadhi ya sauti ambazo hazipo katika lugha ya Kihaya ila zipo katika lugha ya Kiswahili huwapa shida wanafunzi wakati wa kuandika Kiswahili sanifu. Sauti hizo kama zinavyoainishwa katika sura ya pili ni sauti /dh/, /th/, /ngø/, /gh/ na /v/ huchangia kwa kiasi kikubwa katika makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Kwa mfano mwanafunzi huandika ðZaifuð badala ya ðDhaifuð, ðSemaniniø badala ya ðThemaniniø, ðNgoaø badala ya ðNgoaø na ðGorofaø badala ya ðGhorofaø.

Hivyo sauti /v/ ilionekana kutokuwa na athari yoyote kutoka lugha ya Kihaya kwenda lugha ya Kiswahili. Ila mtafiti alipofanya mahojiano na baadhi ya wazazi wenye umilisi wa Kihaya pamoja na Kiswahili, wazazi sita kati ya wazazi kumi waliohojiwa wamedai kuwa wapo wazungumzaji wa Kihaya wanaotumia sauti /b/ badala ya /v/. Kwa mfano wazee wanaozungumza Kihaya husema ðbiongoziø badala ya ðviongoziø na ðbitandaø badala ya ðvitandaø

Hivyo mtafiti aligundua kuwa, kuwepo kwa mfumo tofauti wa sauti wa lugha hizi mbili hupelekea wazungumzaji wa Kihaya kutumia sauti ambazo hukaribiana nazo kimatamshi kwa kiasi fulani wakati wanapojifunza au kuzungumza Kiswahili sanifu. Kwa mfano sauti /g/ hutumika badala ya /gh/, sauti /z/ hutumika badala ya /dh/, sauti /s/ hutumika badala ya /th/ na sauti /ng/ hutumika badala ya /ngø/.

- (ii) Matumizi ya Kihaya muda mwingi kwa wanafunzi, walimu pamoja na jamii kwa ujumla.

Kupitia mahojiano ambayo mtafiti alifanya kwa walimu pamoja na wazazi wenye umilisi wa Kihaya na Kiswahili, mtafiti alibaini kuwa kuna matumizi makubwa ya Kihaya katika mazingira ya shule pamoja na nyumbani. Walimu kumi na watatu kati ya kumi na watano waliohojiwa na mtafiti walidai kuwa Kihaya kimekuwa kama lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shuleni hata nyumbani na hivyo ni vigumu kwa mwanafunzi kuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili. Hii hupelekea pia baadhi ya wanafunzi kutafsiri baadhi ya maneno ya Kiswahili katika lugha ya Kihaya. Kwa mfano mwalimu Latinus wa shule ya msingi Iburu alisema kuwa õmwalimu anapoita majina darasani kama mwanafunzi hajahudhuria wanafunzi watakwambia **hajakuja** hii inatokana na neno la kihaya **tiyaija** lenye maana ya kutohudhuriaõ

Hii husababisha wanafunzi kutopata muda mwingi wa kufanya mazoezi au kuwa na uelewa wa sauti za lugha ya kiswahili ambazo hazipo katika lugha ya kihaya.

Vile vile matumizi ya Kihaya kwa muda mwingi kwa baadhi ya wanafunzi husababisha wanafunzi kuandika maneno ya Kiswahili sanifu kwa kutumia herufi zisizo sahihi na kupelekea kupoteza dhana au maana iliyokusudiwa, kwa mfano kuandika õsamaniõ badala ya õthamaniõ na õgalaõ badala ya õghalaõ.

- (iii) Walimu kutokuwa na taaluma ya fonetiki matamshi.

Mgullu (2010) akimnukuu Laderfoged (1975) anasema fonetiki matamshi ni tawi la fonetiki ambalo huchunguza na kueleza jinsi mtu anavyozungumza. Matinde (2012) anasema fonetiki matamshi ni mojawapo ya matawi ya fonetiki ambalo huchunguza

utamkaji wa sauti mbalimbali za lugha ya mwanadamu. Tawi hili hujikita katika uchunguzi wa:

- (a) Ala za matamshi
- (b) Mahali pa kutamkia
- (c) Namna ya kutamka
- (d) Mikondo ya hewa

Katika mahojiano ambayo mtafiti alifanya na watafitiwa hususani walimu walidai kuwa hata wao wana matatizo katika utamkaji wa baadhi ya sauti. Walimu kumi na mmoja kati kumi na watano walisema kuwa òkuna baadhi ya walimu ambao wakiwa wanaandaa nukuu za somo huwauliza walimu wenzao kama neno fulani lina sauti /r/, /l/ au /h/ ili wamsaidie aweze kuliandika kwa Kiswahili sanifuò. Pia walimu sita kati ya kumi na watano waliohojiwa walisema òwanapozungumza darasani sauti /dh/, /th/, /ngò/, /r/, /gh/, /w/ na /h/ huwa hawazitamki zinavyotakiwa ila hujidhihirisha katika maandishi tu na siyo katika matamshiò.

Mtafiti aliwataka walimu waliohojiwa wataje viungo vilivyomo kinywani ambavyo vinahusika na utamkaji wa sauti /th/, /gh/, /r/ na /h/. Walimu wanne kati ya kumi na watano waliweza kutaja viungo vinavyohusika na utamkaji wa sauti hizo. Hivyo mtafiti alibaini kuwa pamoja na wanafunzi kufanya makosa ya kifonolojia yaweza pia kusababishwa na wale wanaowafundisha lugha ya pili.

Walimu waliohojiwa walipoulizwa kama walimu wenye umilisi mdogo katika sauti za lugha ya Kiswahili wanaweza kutambua makosa ya kifonolojia yanayofanywa na mwanafuzi. Walimu nane kati ya kumi na watano waliohojiwa walisema kuwa

ōkutokana na walimu kutokuwa na ujuzi wa utamkaji wa sauti za lugha ya Kiswahili baadhi yao hushindwa kutambua makosa yanayojitokeza kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili sanifuö. Hivyo hata masahihisho ya makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu hushindwa kuyafanya kwa sababu hushindwa hata kuyabaini.

Mtafiti alibaini kuwa sababu hii inachangia kwa kiasi kikubwa makosa ya kifonolojia kutokana na ufundishaji mbaya wa lugha ya pili ambapo mwalimu hukosa umilisi wa kiisimu katika ufundishaji wa lugha ya pili (Kiswahili). Mwanafunzi hujifunza lugha kwa kusikia mwalimu wake anavyozungumza, hivyo mwanafunzi anaposikia matamshi yenye makosa kutoka kwa mwalimu wake jinsi anavyotamka maneno hayo naye hufanya makosa hayo bila kujua. Mwanafunzi huyachukua makosa yale na kuyachukulia kama maumbo sahihi.

(iv) Mbinu mbaya za ufundishaji wa lugha ya pili

Lugha ya pili siyo lugha ambayo mtoto /mtu aliipata alipoanza kukua na kupata lugha. Hii ni lugha ya kujifunza kwa maana ya kwamba mtu huyo huwa tayari ana lugha nyingine. Wazungumzaji wa Kihaya hutumia Kihaya kama lugha yao ya kwanza na wanapoanza shule ya msingi hujifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili. Hivyo ujifunzaji wa lugha ya pili una mbinu zake. Katika mahojiano yaliyofanywa kati ya mtafiti na wasailiwa hususani walimu, walimu saba kati ya walimu kumi na watano waliohojiwa walisema õhutumia adhabu kama mbinu ya kumfanya mwanafunzi asirudie makosa ya kifonolojia aliyoyafanya katika kazi yake ya maandishiö. Walimu hao walipoulizwa kama mbinu ya adhabu imewasaidia

kupunguza makosa ya kifonolojia kwa wanafunzi? Walimu watano kati ya saba walijibu kwa kusema òpamoja na matumizi ya adhabu kama mbinu ya kufundisha lugha ya pili bado wanafunzi hao wanaendelea kufanya makosa hayoo.

Mtafiti alibaini kuwa walimu hawana mbinu mbadala ya kufundisha wanafunzi lugha ya pili tofauti na kutoa adhabu kwa wanafunzi wanaofanya makosa ya herufi. Makosa katika lugha kwa wanafunzi wanaojifunza lugha hayapaswi kutolewa adhabu bali yanapaswa kuchukuliwa kama hatua ya mwanafunzi kujifunza lugha. Makosa kwa wanafunzi yasichukuliwe kama hali ya mwanafunzi kushindwa kujifunza lugha na kutaka kuondolewa kwa gharama bali yachukuliwe kama sehemu ya hatua ya ujifunzaji lugha (Keshavars 2012).

Watafitiwa hususani walimu ambao ndio warekebishaji wa makosa katika lugha walionekana kutokuwa na uelewa wa kuwa kila mtu anayejifunza lugha lazima afanye makosa na makosa hayo ayatumie kama mrejesho wa kujifunza lugha ya pili. Walimu wanapaswa kujua kuwa makosa kwa mtu yeyote anayejifunza lugha iwe ya kwanza au ya pili lazima yafanyike (makosa kwa mtu anayejifunza lugha ni kitu ambacho hakiepukiki). Vile vile makosa kwa mtu anayejifunza lugha ni muhimu kwa mwalimu pamoja na mwanafunzi mwenyewe kwa sababu makosa katika lugha hueleza uwezo wa utambuzi na kiwango cha uelewa kwa mtu anayejifunza lugha.

Keshavarz (2012) anasema kuwa mbinu ya ufundishaji lugha ya pili iwe ni kurekebisha makosa mara kwa mara kwa kuonesha namna neno linavyopaswa kuwa, pili kutumia zana na marejeleo mbalimbali ya lugha lengwa.



#### **4.5 Mbinu za Kutumia ili Kuwasaidi Wazungumzaji wa Kihaya**

##### **Wanaojifunza Kiswahili Sanifu**

Mtafiti alibaini kuwa, kuna makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Pia mtafiti aliweza kubainisha sababu zinazosababisha kufanyika kwa makosa hayo. Hivyo kuna uhitaji wa kupendekeza mbinu za kutumia ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

Mbinu zilizopendekezwa zimekusanywa nyanjani kutoka kwa watafitiwa ambao ni walimu na wazazi wenye umilisi wa Kihaya na Kiswahili. Mbinu hizo zilizopendekezwa zimekusanywa kwa kutumia njia kuu mbili ambazo ni hojaji na mahojiano ambapo kupitia hojaji watafitiwa walitaja tu mbinu za kusaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu na njia mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watafitiwa ilisaidia kufafanua mbinu hizo zilizotajwa katika hojaji. Mbinu hizo ni hizi ifuatavyo:

- (i) Wazazi, wanafunzi pamoja na jamii nzima ya wazungumzaji wa lugha ya Kihaya kutambua umuhimu wa Kiswahili

Katika utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa wanafunzi wengi huongea Kihaya wawapo shuleni pamoja na nyumbani. Kwa mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na wazazi, wazazi saba kati ya kumi waliohojiwa walisema ðhata baadhi ya dini za kikristo wanafunzi hufundishwa mafundisho ya kidini kwa lugha ya kihaya na hata mtihani wa dini wa darasa la nne hutungwa kwa lugha ya Kihayaö. Mwalimu Mary wa shule ya msingi Kashenge ambaye alijitambulisha kama mwalimu mlezi wa dhehebu la ðRoman Catholicö alisema;

*“.... ni kweli wanafunzi wa darasa la nne wanafanya mtihani wao wa dini  
kwa lugha ya Kihaya ila kwa mwaka huu wameomba mtihani ufanyike  
kwa lugha ya Kiswahili na tayari kitabu cha Katekimu kimetafsiriwa  
kutoka Kihaya kwenda lugha ya Kiswahili”.*

Pia mwalimu Gerevas wa shule ya msingi Kahororo alisema:

*“.... kunapotokea tatizo kwa mwanafunzi akaitwa mzazi, mzazi akifika  
shule ataongea lugha ya Kihaya hata kama mwalimu anayeongea naye  
atakuwa anaongea Kiswahili”.*

Pia mwalimu Kasaba wa shule ya msingi Bugambakamoi alisema;

*“.... hata kwenye mikutano ya wazazi, wazazi waliowengi hutoa hoja zao  
kwa lugha ya Kihaya”.*

Kutokana na hali hiyo jamii, wazazi pamoja na wanafunzi hawaoni umuhimu wa kutumia Kiswahili sanifu katika mawasiliano yao. Wazazi (jamii kwa ujumla) na wanafunzi waelezwe kuwa kwa sasa lugha ya kiswahili ni lugha rasmi na lugha ya taifa nchini Tanzania na nje ya nchi. Kiswahili ni lugha ya ajira, sayansi na teknolojia na shughuli mbalimbali za kiserikali na zile zisizo za kiserikali.

Hivyo wanafunzi wasio na umilisi wa lugha ya kiswahili watakosa haki zao za msingi kutokana na kukosa umilisi katika lugha ya taifa. Wazazi na jamii wakipewa elimu hiyo itasaidia kuwatia moyo wanafunzi kuongea Kiswahili mara kwa mara na hatimaye kuwa na umilisi mzuri wa lugha ya Kiswahili kuliko Kihaya.

(ii) Taaluma ya fonetiki matamshi kutolewa katika ngazi zote za elimu

Taaluma hii inayojihusisha na namna au jinsi ya kutamka sauti za lugha ya mwanadamu bado ni changamoto. Walimu wengi waliohojiwa hasa wenye elimu ya ngazi ya cheti daraja III hawana uelewa wowote wa viungo vinavyohusika na utoaji wa sauti katika kinywa cha mwanadamu na namna au jinsi ya utamkaji wa sauti hizo. Hali hii husababisha utamkaji mbaya wa baadhi ya sauti na hata kushindwa kuziandika. Hivyo wanafunzi wengi hujifunza makosa kutoka kwa mwalimu wao.

Mtafiti anapendekeza kuwa kuna sababu ya taaluma ya fonetiki matamshi kufundishwa kuanzia elimu ya sekondari hasa kidato cha kwanza hadi kidato cha sita ili walimu waliohitimu kidato cha nne na kujiunga na vyuo vya ualimu ngazi ya cheti daraja la III wawe na weledi juu ya utamkaji wa sauti za lugha ya Kiswahili. Vilevile fonetiki matamshi kuwa somo la lazima kwa wanafunzi wote waliopo katika vyuo vya ualimu. Hii itasaidia kuwa na walimu wenye umilisi wa namna ya kutamka sauti mbalimbali wakati wa mawasiliano.

(iii) Matumizi ya mbinu bora za ufundishaji.

Kupitia hojaji zilizogawiwa kwa watafitiwa ambao ni walimu kumi na watano, walimu wote kumi na watano walipendekeza mbinu mbalimbali kuwa mbadala wa mbinu ya adhabu kama ilivyokuwa awali. Mbinu bora za ufundishaji wa lugha ya pili zilizopendekezwa ni pamoja na;

- Utamkaji wa maneno ya kiswahili kwa ufasaha mara kwa mara wakati mwalimu akiwa darasani na nje ya darasa.

- Kufundisha kwa kutumia zana na vifaa mbalimbali ili wanafunzi waelewe kwa haraka sauti fasaha na kuwajengea kumbukumbu za kudumu akilini mwao.
- Kuwapatia wanafunzi orodha mbalimbali za maneno ya Kiswahili sanifu na kuwapatia kazi ya kuyatamka mara kwa mara kwa ufasaha darasani mbele ya wenzao. Haya ni yale maneno yanayomshinda kuyaandika kwa ufasaha.
- Kufanya midahalo mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili ili waweze kutamka maneno kwa ufasaha.
- Kutumia mbinu ya usimuliaji wa hadithi za Kiswahili ili waweze kutamka na kuzungumza Kiswahili sanifu.
- Kuhimiza usomaji wa vitabu mbalimbali vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili kutambua uandishi wa maneno mbalimbali ya Kiswahili sanifu.

#### **4.6 Muhtasari**

Sura hii imeweka wazi malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti. Mtafiti ameweza kuonesha makosa yanayofanywana wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu, sababu za kufanya makosa hayo pamoja na mbinu za kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekeo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inaelezea muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, sehemu ya pili ni mapendekezo na sehemu ya tatu ni hitimisho la utafiti huu.

#### **5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Utafiti huu uliongozwa na malengo mahususi matatu: Kwanza kuainisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu. Pili, kubainisha sababu zinazopelekea wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa katika kujifunza Kiswahili sanifu. Tatu, kubainisha mbinu za kutumia ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili. Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo: Ni makosa gani ya kifonolojiayanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu? Je, nini kinasababisha wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa hayo katika kujifunza Kiswahili sanifu? Mbinu gani zitumike ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

Utafiti huu umegundua kuwa kuna makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Makosa hayo ni matumizi

ya sauti mbadala hasa kwa zile sauti ambazo hazipo katika mfumo wa sauti za lugha ya Kihaya ila zipo katika lugha ya Kiswahili sanifu, kuchanganya sauti hasa kwa sauti za Kiswahili sanifu zenye ufanano wa karibu kimatamshi, udondoshaji wa sauti na uchopekaji wa sauti wakati wa kuandika Kiswahili sanifu. Makosa haya ya kifonolojia yanasababishwa na tofauti kubwa ya mfumo wa sauti za Kihaya na Kiswahili ambao huathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kihaya. Vile vile walimu hasa wa ngazi ya cheti kutokuwa na taaluma ya fonetiki matamshi. Pia walimu, wazazi na wanafunzi kutumia muda mwingi kuongea Kihaya badala ya Kiswahili. Mwisho, ni matumizi ya mbinu mbaya za ufundishaji wa lugha ya pili.

Kutokana na uwepo wa makosa ya kifonolojia yanayofanywana wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu, mtafiti amependekeza mbinu mbalimbali za kuweza kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu. Mapendekezo hayo yalizingatia maoni ya watafiti wake aliofanya nao mahojiano ya ana kwa ana. Mbinu hizo ni pamoja na wazazi, walimu, wanafunzi pamoja na jamii nzima kutambua umuhimu wa lugha ya Kiswahili, taaluma ya fonetiki matamshi kutolewa katika viwango vyote vya elimu na kutumike mbinu bora za ufundishaji. Mbinu hizi zitasaidia kupunguza makosa ya kifonolojia kwa mwanafunzi mwenye L1 anayejifunza L2.

### **5.3 Mapendekezo ya Utafiti**

Kwa kuwa utafiti huu haukushughulikia makosa yote yanayokumba wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu, tunapendekeza sehemu zifuatazo kushughulikiwa na tafiti zingine. Kwanza, makosa ya vipengele vingine vya kiisimu kando na fonolojia yaachunguzwe. Pili, mbinu zaidi za kukusanya data zihuzishwe

katika tafiti za usoni; matokeo yatakayotokana na mbinu hizo yanaweza kutumiwa kulinganisha matokeo ya utafiti huu uliotumia mbinu tatu. Tatu, sampuli za wanafunzi kutoka viwango tofauti tofauti zitumike kwa nia ya kulinganisha hatua za kujifunza lugha zao lengwa. Hali kadhalika, tafiti za jinsi hii zifanywe katika maeneo mbalimbali yenye L1 tofauti kwa minajili ya kulinganisha matokeo haya na hata kubaini ikiwa matokeo ya jinsi hii yana umajumui wowote kwa kila anayejifunza lugha ya pili.

#### **5.4 Hitimisho**

Kupitia kufanyika kwa utafiti huu, matokeo yake yamedhihirisha makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu, visababishi vya athari hizo mbinu za kutumia ili kuwasaidia wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya katika kujifunza Kiswahili sanifu yafaa yashughulikiwe kwa kuwa kila kosa lina kisababishi chake.

### MAREJELEO

- Ali, N. (2013). Kiswahili Jukwaani. Blogu ya Kujifunza lugha na Fasihi ya Kiswahili na Waswahili. Retrieved on 11<sup>th</sup> July 2018 from: <https://kiswahilijukwaani.blogspot.com/2013/12/kiswahili-ni-nini.html>.
- Babbic, E. (1999). *The Basics of Socil Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Bassetti, B., na Atkinson, N. (2015). *Effects of Orthographic Forms on Pronunciation in Experienced instructed Second language learners*. London: Cambridge University press.
- Chully, M. (2017). *Phonological Structure in Kihaya* at [chullytzed.blogspot.com](http://chullytzed.blogspot.com).
- Corder, S. (1967). The significance of learner's errors. *International Review of Applied Linguistics*, 5(4), 161-170.
- Corder, S. (1971). *Idiosyncratic Dialects and Error Analysis*. In J.C Richards (Ed), *Error Analysis: Perspective on second Language learning*. London: Longman.
- Corder, S. (1974). *Error Analysis*. In J. Allen and S. Corder (eds). Oxford: Oxford University Press.
- Corder, S. (1978). *The Significance of Learners' Errors*. In J.C. Richards. *Error Analysis: Perspective on Second Language Acquisition*. London: Longman.
- Dulay, H., na Burt, M. (1974). *You Can't Learn Without Goofing*. In J.C Richard (Ed) *Error Analysis*. London: Longman.
- Gass, S., na Selinker, L. (1994). *Second language Acquisition: An Introductory Course*. In N. Abisamra (2003). *An analysis of Errors in Arabic Speakers' English writing*. American University of Beirut. America.



- Gass, S., na Selinker, L. (2008). *Second language Acquisition: An Introductory Book*. (3<sup>rd</sup> ed). London: Routledge.
- Jain, M. P. (1974). *Error Analysis: Source, Cause and Significance*. In J.C Richards (Ed), *Error Analysis. Perspective on Second Language Learning*. London: Longman.
- Josephine, N. (2015). *Athari za Lugha ya Kinyamwezi katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
- Keshavarz, M. H. (2012). *Contrastive Analysis and Error Analysis*. Teheran: Rahnama Press.
- Khalfan, A. S. (2011) Number and Agreement Errors Made by Native Arabic Learners of Kiswahili: The case of Libyans Students in Institute of Kiswahili and Foreign Language (IKFL) - Zanzibar. (Unpublished) M.A. Dissertation of the University of Dar es Salaam, Tanzania.
- Kombo, D. K na Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction*: Nairobi: Paulines Publication Africa.
- Kothari, C. R. (1990). *Research methods, Techniques and Procedures*. London: London University press.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.
- TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Masebo, J. A. na Nyangwine, C. N. (2012). *Nadharia ya Lugha: Kiswahili 1: Kidato cha 5 na 6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Massamba, D. P. B. (1986). On the Influence of Local Language on Kiswahili. The Case of Mara Region in Tanzania. In Ontieri, J. O (2013). Phonological

- Influence of First Languages on Kiswahili: A Case Study of Kenyan Bantu Languages. Maasai Mara University. Narok, Kenya.
- Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500 BK*: Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Massamba, D. P. B. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D. P. B. (2012). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA); Sekondari na Vyuu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matinde, R. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publisher Ltd
- Mradi wa Lugha Tanzania, (2009). *Atlas ya Lugha Tanzania*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mudhune, E. S. (1994). A constructive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo Speakers. In Ontieri, J.O (2013). *Phonological Influence of first Languages on Kiswahili: A Case Study of Kenyan Bantu Languages*. Maasai Mara University. Narok, Kenya.
- Nchimbi, A. S. (2008). OFC 008: Kiswahili. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Njeru, M. G. (2013). *Dialect and Learning of English as a Second Language in Kenya*. Nairobi: Sciedu Press.

- Richards, J. C. (1971). *A Non-Contrastive Approach to Error Analysis*. In J.C Richards (Ed), *Error Analysis. Perspective on Second Language Learning*. London: Longman.
- Richards, J. C. (1974). Errors Analysis and Second Language Strategies. Paper presented at Midis du GREDIL, Université Laval, Sainte-Foy, Quebec: Canada.
- Richard, J. C., na Rodgers, T. S. (1986). *Approaches and Methods in Language Teaching*. New York: Cambridge University Press.
- Richards, J. C., na Sampson, G. (1974). *The Study of Learners English*. In J.C Richards (Ed), *Error Analysis. Perspective on Second Language Learning*. London: Longman.
- Taylor, B. P. (1975). *The Use of Overgeneralization and Transfer Learning Strategies by Elementary and Intermediate Students of ESL Language Learning*. Michigan: University of Michigan.
- Theophil, P. (2012). *Matumizi ya Lugha na Utambulisho wa Jamii ya Wahaya waishio Dar es Salaam*. Tasnifu ya M.A Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Tremblay, A. (2017). How Does Mother Tongue Affects Second Language Acquisition Improving Literacy and Communication Language Magazine.
- Wenceslaus, M. (2015). Athari za Lugha ya Kijita katika Kujifunza Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Williman, N. (2011). *Research Methods; The Basic*. New York: Routledge Taylorand Francis Group.

## VIAMBATANISHO

### RATIBA YA UTAFITI NA GHARAMA ZA UTAFITI

#### 6.0 Ratiba ya Utafiti

Utafiti huu umekamilika kwa kupitia katika hatua kuu tatu (3), ambazo ni matayarisho ya pendekezo la utafiti, ukusanyaji data na uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Kwa hiyo ratiba ya mtafiti itakuwa kama ifuatavyo:

<b>MWEZI</b>	<b>KAZI ITAKAYOFANYIKA</b>
<b>Agosti - Septemba 2018</b>	Uandaaji wa pendekezo la utafiti na uwasilishaji wa pendekezo kwa msimamizi wa utafiti
<b>Oktoba - Novemba 2018</b>	Ukusanyaji na uchanganuzi wa data.
<b>Disemba 2018 – Januari 2019</b>	Uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kwa msimamizi wa utafiti.

#### 6.1. Makadrio ya Gharama za Utafiti

Hizi ni gharama zilitumika tangu hatua ya uandaaji wa pendekezo la utafiti, ukusanyaji na uchanganuzi wa data hadi uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

<b>Namba</b>	<b>Shughuli</b>	<b>Kiasi cha fedha</b>
1.	Usafiri	400,000/=
2.	Chakula	250,000/=
3.	Vifaa na uchapishaji	900,000/=
4.	Gharama nyinginezo	430,000/=
	Jumla	1,980,000/=

**HOJAJI/ DODOSO**

Mimi Frederick Felician, mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninalenga kufanya utafiti kuhusu athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Kazi hii ni kwa ajili ya kitaaluma. Mchango na maoni utakayotoa yatakuwa na manufaa makubwa kwangu na wale watakaosoma kazi hii. Maoni yako yatatunziwa siri kubwa, Karibu.

**A. Hojaji upande wa wanafunzi**

Weka alama ya [ ] kwenye jibu unaloona ni sahihi.

1. Wewe ni Mhaya?
  - (a) Ndiyo
  - (b) Hapana
2. Unajua Kuongea lugha ya Kihaya?
  - (a) Najua kabisa
  - (b) Najua kidogo
  - (c) Sijui kabisa
  - (d) Sijui hata kidogo
3. Ni lugha ipi unaitumia unapokuwa katika mazingira ya shule?
  - (a) Kihaya
  - (b) Kiswahili
4. Ni lugha ipi unaitumia unapokuwa mazingira ya nyumbani?
  - (a) Kihaya
  - (b) Kiswahili
5. Katika kujifunza kwako Kiswahili kuna maneno yoyote yanayokupa shida kuyaandika au kuyatamka wakati unapoandika au kuongea Kiswahili?

(a) Ndiyo

(b) Hapana.

6. Kama jibu la swali la 5 ni ndiyo, basi taja maneno matano ya Kiswahili yanayokupa shida kuyaandika au kuyatamka wakati unapojifunza Kiswahili.

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(v)

### **B. Hojaji upande wa walimu**

Weka alama ya [ ] kwenye jibu unaloona ni sahihi.

1. Je, uwezo wako kama mwalimu wa kuzungumza na kuelewa Kihaya ni wa kiwango gani?
  - (a) Mzuri sana
  - (b) Mzuri
  - (c) Kiasi
  - (d) Mbaya
  - (e) Mbaya sana
2. Wanafunzi katika shule yako wanchanganya baadhi ya herufi za Kihaya na zile za Kiswahili?
  - (a) Nakubali kabisa
  - (b) Nakubali
  - (c) Sikubali
  - (d) Sikubali kabisa
3. Walimu shuleni kwako hutumia Kihaya katika mawasiliano yao?
  - (a) Hutumia sana
  - (b) Hutumia kiasi

- (c) Hawatumii
- (d) Hawatumii kabisa

4. Wanafunzi hufanya makosa yoyote yanayosababishwa na lugha ya kihaya wakati wa kuandika au kuzungumza lugha ya kiswahili?

- (a) Ndiyo
- (b) Hapana

5. Kama jibu hapo juu ni ndiyo, basi andika maneno kumi (10) ya Kiswahili yanayowapa shida wanafunzi kuyaandika au kuyatamka wakati wanapozungumza lugha ya Kiswahili fasaha.

- (i)
- (ii)
- (iii)
- (iv)
- (v)
- (vi)
- (vii)
- (viii)
- (ix)
- (x)

7. Matamshi ya maneno ya Kihaya huathiri vipi wanafunzi wa kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili? Eleza kwa mifano.

8. Ni sababu zipi zinazosababisha Kihaya kuathiri matamshi ya lugha ya Kiswahili?

9. (a) Makosa hayo unayarekebisha vipi?

(b) Taja mbinu unazoweza kutumia kurekebisha athari za kimatamshi za Kihaya katika

Kujifunza Kiswahili

**C. Hojaji kwa wazazi wamilisi wa Kihaya na Kiswahili**

1. Je, wazazi wantumia lugha ipi kati ya hizi kuwasiliana na wanafunzi wanapokuwa nyumbani?
  - (a) Kihaya
  - (b) Kiswahili
2. Je, kuna namna yoyote ya kimatamshi ya lugha ya Kihaya huathiri matamshi ya Kiswahili hasa kwa wanafunzi wetu?
  - (a) Ndiyo
  - (b) Hapana
3. Kama jibu la swali la pili ni ndiyo, unaweza kutaja makosa hatamatano ambayo wanafunzi Wahaya huyafanya wakati wanapotamka maneno ya Kiswahili?
  - (i)
  - (ii)
  - (iii)
  - (iv)
  - (v)
4. Kama athari za kimatamshi za Kihaya zipo kwa wanafunzi Wahaya wanaojifunza Kiswahili, unadhani athari hizo husababishwa na nini?
5. Tunaweza kufanya nini ili kuweza kuepukana na athari za kimatamshi za lugha ya Kihaya kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili?